**Adaiwa** kumchoma mwanawe kisa wizi ugali nyama wa bibi

UKURASA 2



**Shahidi** akwamisha kesi ya Ole Sabaya sababu ya sikukuu

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe

Jumatano Julai 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580648

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# MARUFUKU

• **WAZIRI** akataza silaha kwenye mikusanyiko, aagiza ukaguzi milangoni...*Endelea ukurasa 2*

Vituo vya mabasi



Viwanjani



Baa



Harusini



Sokoni



Daladala






Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene.

# RC Mwanza apiga 'stop' kongamano CHADEMA

UKURASA 2

## Samia atoa milioni. 100/- Machinga Complex

UKURASA 3

MICHEZO YANGA YASISITIZA HAITABEBWA CAF UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu madhehebu ya Answal Sun, wakishiriki swala ya Sikukuu ya Eid Al Adha, kwenye uwanja wa Mtekelezo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Marufuku silaha katika mikusanyiko

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amepiga marufuku ya kuingia na silaha kwenye maeneo ya starehe kama baa, kumbi za muziki, harusi na mengine yenye mkusanyiko.

Katika kuhakikisha angalizo hilo linazingatiwa, ameagiza ni lazima kuwapo utaratibu wa wahusika na maeneo hayo kufanya ukaguzi mlangoni kabla ya watu kuingia ndani ya maeneo hayo tajwa.

Simbachawene alitoa agizo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kukamilisha ziara yake ya siku mbili mkoani Iringa.

Ziara hiyo ilijumuisha kutembelea maeneo mbalimbali kikiwamo kiwanda cha Hong Wel International kilichoko mjini Mafinga.

Alisema wizara inaona kuna jambo la kujifunza kupitia tukio la mauaji yaliyotokea kwenye baa mkoani Dar es Salaam.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, maeneo ya Sinza mkoani Dar es Salaam, kijana aliyetambulika kwa jina la Alex Koroso, alidaiwa kumuua kijana mwenzake kwa na bastola kisha kujiua.

Simbachawene alisema kuwa kutokana na tukio hilo wanaona suala la umilikishaji wa silaha na utunzaji wa silaha lina dosari kubwa katika maeneo mengi.

Alisema anayemilikishwa silaha ni lazima awe ni mtu mwenye akili timamu na siyo mtu mwenye pesa asiye na akili timamu.

Simbachawene alisema umejitokeza utaratibu usio mzuri kwamba mtu akishakuwa na pesa tu, pasipokuwapo tishio lolote la usalama wake, anakimbilia kununua silaha, tena pasipo kufuata utaratibu wowote wa umilikishaji wa silaha.

"Mtu anayepewa kibali cha umiliki wa silaha lazima awe na akili timamu na awe ni yule mwenye tishio la kiusalama na siyo mtu kuwa na pesa lazima kumiliki silaha.

"Kwa sasa imejitokeza tabia ya baadhi ya vijana kumiliki silaha kama fasheni na wengi wao wamekuwa wakienda maeneo ya starehe wakitamba kwa kuonyesha silaha hizo wanazomiliki hadharani kuwa 'mimi nina bastola hapa', jambo ambalo ni kinyume cha sheria inayozingatiwa katika umiliki wa silaha," alionya.

Alisema kumiliki silaha siyo sifa ama ufahari bali heshima kwa wamiliki wa silaha ni kuheshimu matumizi na vibali vyake.

Alisema wapo baadhi ya watu wanamiliki silaha na hawajulikani kutokana na kupata silaha hizo kupitia kwa madalali.

Alisema wizara yake imeanza mchakato wa kutambua wamiliki wa silaha na tayari baadhi ya watu waliohusika na utoaji wa vibali vya silaha wamesimamishwa ili kupisha uchunguzi na ripoti kamili ya mchakato wa umilikishaji wa silaha inaandaliwa.

Katika ziara yake hiyo, waziri huyo pia aliwataka wawekezaji wanaofanya shughuli zao katika Wilaya ya Mufindi, kuendelea kufanya shughuli zao kwa utulivu na kuacha kufanyiana visa na kupigana.

# RC Mwanza apiga 'stop' kongamano CHADEMA

**Na Richard Makore,** MWANZA

SIKU moja baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutangaza kufanya kongamano la kudai Katiba Mpya jijini Mwanza leo, Mkuu wa Mkoa huo, Robert Gabriel, amepiga marufuku mikusanyiko isiyo ya lazima ili kujikinga na ugonjwa wa corona.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Gabriel alisema mikusanyiko isiyo ya lazima ikiwamo sherehe haitakiwi.

Hata hivyo, alisema nyumba za ibada zinaruhusiwa kuendelea na ibada, lakini waumini wote waendelee kuchukua hadhari ikiwamo kuvaa barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka.

Alisema serikali imeshaanza mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona na sasa imefanya maboresho ili kuhakikisha wanalipa mkazo suala hilo.

Alisisitiza suala la elimu ikiwamo uvaaji wa barakoa ili kuzuia kuambukiza wengine na mtu mmoja mmoja kujikinga.

Wakati kiongozi huyo wa mkoa akitoa agizo hilo, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA), John Pambalu, amesisitiza kwamba mkutano wao wa leo utafanyika kama ulivyopangwa.

Alisema jana kuwa wamechukua tahadhari ikiwamo kuvaa barakoa ili kuhakikisha wanajikinga na ugonjwa wa corona.

Juzi, mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, alisema jijini Mwanza kuwa tatizo la corona ni kubwa, lakini hatua zinazochukuliwa na serikali zimekuwa hafifu kwa kuwa hakuna bajeti yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kupambana nalo.

Alisema gharama za kumhudumia mgonjwa mmoja katika hospitali za kawaida kwa wiki zinafikia Sh. milioni 2.5 huku hospitali za binafsi zikitoza mpaka Sh. milioni 15 kwa mgonjwa mmoja.

Mbowe alisema ugonjwa wa corona ni janga la dunia na kwamba serikali ilitakiwa kulichukulia hivyo na kuweka mikakati na bajeti ya kutosha badala ya kuendelea kufanya alichokiita mizaha.

# Amchoma moto mwanawe madai wizi ugali nyama

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Mtwara, linamshikilia Muwaza Abeid (29) kwa tuhuma za kumchoma moto na kumjeruhi mwanaye mwenye umri wa miaka minane ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili Shule ya Msingi Naliendele, kwa madai ya kuiba ugali nyama wa bibi yake.

Akizungumza na Nipashe jana kwa simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Mark Njelwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kwamba mama huyo anashikiliwa kwa ajili ya kuhojiwa kabla ya sheria kuchukua mkondo wake.

"Hili tukio ni kweli limetokea mtoto amejeruhiwa kwa kuchomwa moto vibaya mkono wa kulia na mama yake mzazi kisa alidai kaiba ugali nyama ulioachwa kwa ajili ya bibi yake," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana mkoani humo zilizothibitishwa na Ofisa Ufuatiliaji na Tathimini wa Kituo cha Msaada wa Sheria Manispaa ya Mtwara Mikindani, Judith Chitanda, tukio hilo lilitokea Julai 3, mwaka huu, na mama yake kumficha ndani huku akimtibu kienyeji.

Alisema baada ya kumhoji alisema mwanawe huyo alikula ugali na nyama ambao ulikuwa amewekewa bibi yake aliyekuwa amekwenda shambani.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, bibi aliporudi alimwuliza mtoto huyo kama amekula hicho chakula na alikiri kula, lakini mama yake alimfunga mikono yote miwili kwa kutumia majani ya mnazi huku akimtisha. Alisema mtoto huyo aliangukia eneo lenye moto na majani hayo kushika moto na kumuunguza mkono wa kulia.

"Muda mwingi mama yake alikuwa analia kujutia tukio hilo. Anaomba jamii imsamehe na hakutegemea mwanawe anaweza kuungua kwa kiasi hicho na kwamba ni mtundu kwa kuwa amekuwa na tabia ya udokozi hadi fedha na siku hiyo alitoka kwa shangazi akiwa ameshakula chakula cha mchana lakini kutokana na udokozi akala chakula cha bibi yake," alisema.

Kamanda Njelwa alisema mtoto huyo anaendelea na matibabu hospitalini.

HABARI KITAIFA

# Shahidi akwamisha ushahidi kesi ya Sabaya kisa sikukuu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa pili wa upande wa Jamhuri Numan Jasin (17) katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (34), ameshindwa kutoa ushahidi kutokana na sababu za kiimani kwa kuwa jana ilikuwa sikukuu ya Eid el Hajj.

Sabaya na wenzake wawili Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wanakabiliwa na kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha katika Mahakama ya hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha.

Juzi, Jasin alianza kutoa ushahidi wake katika kesi ya jinai namba 105, inayowakabili watu hao.

Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, akizungumza jana mahakamani hapo, alidai kwamba shahidi wa pili alishindwa kufika mahakamani kumalizia kutoa ushahidi wake, kwa kuwa yupo katika maadhimisho ya sikukuu ya Eid, hivyo kutokana na imani yake asingeweza kufika mahakamani kuendelea na ushahidi.

"Mheshimiwa Hakimu tunaomba shauri liahirishwe kusikilizwa kwa kuwa shahidi wetu wa pili ameshindwa kufika mahakamani kumalizia kutoa ushahidi wake kwa kuwa yupo kwenye maadhimisho ya sikukuu ya Eid.

"Kwa kuwa ni suala la imani na ameshindwa kufika hapa na sisi tunatambua umuhimu wa imani za watu, tunaomba mahakama yako tukufu kuahirisha kusiliza shauri hili hadi Julai 22, mwaka huu," alidai.

Baada ya kusikiliza ombi hilo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo, aliahirisha kusilizwa kwa kesi hiyo hadi kesho majira ya saa 2:00 asubuhi.

Juzi, shahidi huyo akihojiwa na Wakili Kweka, alidai kuwa Februari 8, mwaka huu, majira ya saa 11:00 jioni, akiwa katika duka la mjomba wake (Mohamed Saad), alikwenda dada mmoja (hakumtaja jina), kununua kapeti la sebuleni. Alidai wakati wa kulipa fedha, alisogea sehemu ya kulipia (kaunta) na alitaka kulipia bidhaa hiyo kwa Dola 100 za Kimarekani lakini alimwambia kwamba hawapokei dola bali fedha za Kitanzania.

"Bidhaa aliyokuwa anataka kununua ilikuwa na thamani ya Sh. 200,000. Tulimwambia aende kubadilisha benki na alikwenda. Baada ya muda alirejea akalipia bidhaa hiyo, nikampatia risiti na kisha aliondoka," alidai.

Februari 9, mwaka huu, shahidi huyo alidai kwamba dada huyo alikwenda dukani kwao kununua tena kapeti dogo, walimuuzia na kumtapia risiti na alivyoondoka baada ya dakika 10, kundi la watu sita walifika na kusimama nje ya duka wanaume wakiwa watano na mwanamke mmoja.

"Watu hao waliingia ndani ya duka na yule mwanamke alikaa nje. Wanaume waliingia kama wateja na baada ya muda walianza kupekua mapazia na mmoja wa wanaume hao, alifika pale kaunta na kuniambia nimpigie simu mwenye duka (Mohamed Saad) kuwa kuna wateja wanahitaji mapazia kwa bei ya jumla,

"Nilimpigia simu kumweleza kwamba wateja wake wa jumla wanamhitaji dukani. Aliniambia kuwa yuko mbali hawezi kufika dukani na mmoja kati ya watu hao, aliniambia nimpigie simu kumwambia kwamba wao ni wateja.

"Baada ya mjomba kusema yuko mbali na hawezi kuja, kundi lingine la watu wanne nje ya duka, wanaume watatu na mwanamke mmoja, waliingia ndani na kufunga mlango wa duka. Baada ya kuingia, mmoja kati ya wanaume hao, alisogea tena pale kaunta na kuniambia kwa nimpigie tena simu mjomba kumwambia maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wapo dukani kwake wanamhitaji afike haraka," alidai Shahidi huyo.

Shahidi huyo, aliendelea kudai kuwa baada ya kumpigia simu, mhusika alimjibu kwamba bado yupo mbali, hivyo hawezi kufika dukani hapo na alikata simu na baada ya hapo, mmoja wa wanaume hao (baunsa) alimwamuru kupiga simu kwa mara nyingine.

Alidai kuwa mmoja wa wanaume waliokuwa dukani hapo, walinyanganya simu yake na kuweka "loud spiker" na Mohamed alipokea simu na mtu huyo kumwambia kuwa ndani ya dakika tano wanataka awe amefika vinginevyo watamtafuta Arusha nzima.

"Baada ya Mohamed kukata, mmoja wa wanaume hao aliamuru tuwekwe chini ya ulinzi na walimpekua mmoja wa mfanyakazi aliyekuwapo dukani anaitwa Ali Saad na baada ya hapo walitupiga sana hasa makofi kwenye sehemu za masikio na usoni. kwa kweli walitupiga kipigo kikubwa," alidai.

Aidha, shahidi huyo alidai kuwa kiongozi aliyekuwa akiliongoza kundi la watu hao (Sabaya), aliwaagiza walinzi wake wamsachi na kumweka chini ya ulinzi huku wakimwambia kuna Dola la Kimarekani 70,000 ziliibiwa Moshi mkoani Kilimanjaro na walishirikiana na dada yule aliyekwenda kununua kapeti dukani hapo.

"Sabaya alichukuwa simu yangu akawa anarekodi wakati akinihoji alitaka nitoe majibu ambayo yatampendeza. Nilipotoa majibu tofauti na aliyotaka yeye, aliwagiza walinzi wake waendelee kunipiga hadi hapo nitakapotoa majibu ya kumfurahisha.

"Alitaka nikubali kwamba dukani kwetu tunabadilisha fedha za kigeni na tulishirikiana na dada yule aliyekuja dukani kuiba fedha ambazo ni Dola za Kimarekani 70,000 wakati si kweli," alidai.



Wafanyabiashara ambao wengi wao ni waathirika wa moto katika soko la Kariakoo, wakiendelea na shughuli zao kama kawaida baada ya kuhamishiwa katika soko la Machinga Complex, jana. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Samia atoa mil. 100/- ujenzi Machinga Complex

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. milion 100 kwa ajili ya ujenzi wa paa la kisasa la kuzuia jua na mvua katika eneo linalotumiwa na waathirika wa moto 1,800 wa soko la Kariakoo, waliohamishiwa Machinga Complex.

Akizungumza na wafanyabiashara hao alipotembelea soko hilo jana, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alithibitisha kupokea fedha hizo na kubainisha kuwa ujenzi wa paa hilo utaanza mara moja.

Alisema baada ya juzi kuwatembelea na kuwasikiliza wafanyabiashara hao, Rais Samia aliona tatizo hilo na alipomwuliza kiasi cha fedha kinachohitajika, alimjibu kuwa ni Sh. million 62 kwa paa la turubai lakini kwa kutambua umuhimu wa wafanyabiashara hao, alitoa Sh. milioni i 100 ili lijengwe paa la kudumu.

"Rais Samia aliona nilivyokuja kuwaona jana (juzi) akasema naona mnahangaika na changamoto ile ya wafanyabiashra wetu wapate kivuli. Nikamweleza kwamba kunahitajika Sh. million 62 ili wawekewe paa la kivuli. "Akasema mnawekaje kivuli, nikasema tunatarajia kuweka kivuli cha maturubai ambayo yanaweza kudumu kwa miaka mitano, akasema hapana pigeni hesabu za kuwajengea kuvuli cha kudumu, kama ni kujenga soko liwapo mpauwe kwa bati," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya kupewa maelekezo na Rais, alikaa na makandarasi wa Suma JKT, kwa ajili ya kujadiliana na kueleza kuwa gharama zitakazotumika katika ujenzi huo ni Sh. million 100 na fedha hizo zimeshapatikana, hivyo ujenzi utaanza mara moja.

Aidha, Makalla alibainisha kuwa serikali pia inashuhulikia suala la kuboresha vizimba, na vipo katika uandaaji, vitakapokamilika wafanyabiashara watakabidhiwa na kuwekwa walipo ili waendelee na biashara zao.

FARM AFRICA

## TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Farm Africa limekuwa likifanya kazi nchini Tanzania tangu 1990 kama Asasi isiyo ya Serikali (NGO) chini ya Sheria ya NGO na ikiwa na cheti cha usajili no. I-NGO / 0008750. Madhumuni ya muda mrefu ni kusaidia kupunguza umasikini kwa kuendeleza njia zenye msingi wa jamii za kuboresha uzalishaji wa kilimo na matumizi endelevu ya ardhi nchini Tanzania.

Farm Africa ni shirika la kimataifa lenye ubunifu ambao hupunguza umasikini vijijini katika ukanda wa Africa mashariki kwa kusaidia wakulima wadogowadogo kukuza uzalishaji wa tija kwa kuongeza mavuno, kupata na kufikia masoko ya uhakika, na kuongeza thamani ya mazao huku tukiwa na kipaumbele cha juu katika uendelevu na utunzaji wa mazingira.
Farm Africa inafanya kazi chini ya Mpango Mkakati wa kipindi cha 2021-2025 wenye dhamira ya kuboresha ustawi wa jamii kupitia Kilimo

Mnamo tarehe 12 Julai 2021, Farm Africa iliigia makubaliano na taasisi ya Mpango wa Chakula Duniani (WFP) wenye thamani ya shilling 1,460,739,588 / = kama ruzuku ya kutekeleza mradi wa miezi kumi na mbili (12) ambao utazingatia mnyororo wa thamani ya mtama mkoani Dodoma. Mradi huo unakusudia kuhakikisha kwamba "Wakulima wadogo walengwa katika wilaya za mkoa wa Dodoma watakuwa wameongeza upatikanaji wa masoko ya kilimo ifikapo 2030, kuboresha usalama wa chakula na lishe kupitia uzalishaji bora na mapato (lengo la SDG 2.3)."

**Mradi huo umelenga matokeo yafuatayo:**

1. Wakulima walengwa wanafaidika na mnyororo wa thamani wa WFP na kuboresha upatikanaji wa masoko ya uhakika na yenye tija.
2. Wakulima wadogo walengwa wananufaika na upatikanaji bora wa huduma na bidha za kilimo himilivu ili kuongeza uzalishaji na mapato na kupunguza athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi.
3. Wakulima wadogo walengwa wananufaika kutokana na upatikanaji mkubwa wa miundombinu ya uhifadhi katika kaya na jamii ili kupunguza upotevu wa mavuno baada ya kuvuna na kuboresha ubora wa mazao yaliyovunwa.
4. Kuongeza usawa wa kijinsia na ushiriki wa vijana katika kufanya maamuzi yanayohusiana na uzalishaji wa kilimo na shughuli za uuzaji

Mradi huu utatekelezwa katika wilaya zote za mkoa wa Dodoma. Ilani hii ni katika kufuata kanuni ya mashirika yasiyo ya kirikali (Marekebisho), 2018 GN609 ya 19 Oktoba 2018.

Kupata habari zaidi tafadhali tuma barua pepe kwenda infotanzania@farmafrica.org

# HABARI KITAIFA

## Kigogo CCM matatani tuhuma kuuza maeneo

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WATU watano akiwamo Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kata ya Mapinga, Omari Shabani, wamewekwa chini ya ulinzi kwa tuhuma za kuuza maeneo kinyume na sheria na kusababisha migogoro katika eneo la Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo.

Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ameagiza watuhumiwa hao kuhojiwa kwa tuhuma za kuhusika na utapeli wa kuuza maeneo.

Lukuvi alitoa agizo hilo jana akiwa katika mkutano na wananchi eneo la Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo kusikiliza kero za migogoro ya ardhi na kuzitolea ufumbuzi. Alitoa amri ya kuwekwa chini ya ulinzi watuhumiwa hao baada ya kutajwa na wananchi walioshiriki kwenye mkutano huo wakidaiwa kuhusika kuuza maeneo kiholela na kusababisha migogoro ya ardhi.

Watuhumiwa hao ni Omari Shabani ambaye ni Katibu Mwenezi wa Kata ya Mapinga, Ramadhani Rashidi aliyekuwa katibu wa kitongoji cha Kiembeni, William Urio, Muhoni Marwa na Mwanahamis Habibu. Lukuvi alimuagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Bagamoyo kufanya mahojiano ya kina na watuhumiwa hao na wakibainika hatua za kisheria zichukuliwe kukomesha migogoro ya ardhi.

Alisema kwenye chama hawawezi kuwatetea matapeli na watakaobainika watachukuliwa hatua kwa kuharibu taswira ya chama. Pamoja na wananchi kuwataja watuhumiwa hao pia Diwani wa kata ya Mapinga Chandika Dismas pamoja na baadhi ya viongozi walikiri kiongozi huyo wa Chama kuwa na jopo lake ambalo linashiriki kuuza maeneo na kuchochea migogoro katika eneo hilo.

Kaimu Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bagamoyo, Abubakari Mlawa, alikiri kupata taarifa za tuhuma za viongozi hao na kusema; "Kama chama tuhuma zilitufikia na taratibu za kufuatilia tuhuma hizo zinaendelea."

Alisema wanatarajia kukaa vikao na kujadili tuhuma za viongozi hao na atakayebainika atavuliwa nafasi ya uongozi kwa kuwa kata hiyo imekua kinara wa migogoro ya ardhi.

Mlawa ameongeza kuwa hatua hizo si kwa viongozi wa chama pekee hata viongozi wa serikali waliopata dhamana za uongozi wao kupitia CCM ambao wametuhumiwa nao watachukuliwa hatua kali.



Mtaalamu wa mifumo ya kompyuta wa taasisi ya Vodacom Foundation, Omari Amir akielekeza jinsi ya kutumia kompyuta kwa mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Jokate Mwegelo ya wilayani Kisarawe, Mkoa wa Pwani, baada ya taasisi hiyo, kukabidhi msaada wa kompyuta 15 kwa shule hiyo, ikiwa na lengo la kuhakikisha wanafunzi wanapata maudhui ya elimu bure kupitia tovuti ya e-fahamu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## TRC yaona fursa Simba na Yanga

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Reli (TRC) limetenga treni maalum kwa ajili ya wapenzi wa mpira kwenda kushuhudia mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga inayotarajiwa kuchezwa mkoani Kigoma Jumapili ya wiki hii.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TRC, treni hizo zinatarajia kuanza kusafirisha abiria watakaokwenda kushuhudia mechi hiyo kesho kutwa.

Kwa mujibu wa TRC, nauli zitakazotumika kwa watakaotumia usafiri wa treni hizo kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma ni Sh. 150,000 (kwenda na kurudi) kwa daraja la pili kulala.

Daraja la pili kukaa ni Sh. 120,000 wakati daraja la tatu kukaa ni Sh. 100,000 na tiketi zake zinapatikana katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora na Kigoma.

Simba na Yanga, watani wa jadi, watachuana katika mechi hiyo ya fainali ya Kombe la Shirikisho.

Mechi hiyo inatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa, Simba wakisaka ushindi wa kwanza dhidi ya Yanga msimu huu baada ya kufungwa na watani wao visiwani Zanzibar kisha wakatoka sare ya 1-1 mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara kabla ya kufungwa goli 1-0 mzunguko wa pili.

## TAHLISO wamwangukia Samia mikopo ya HESLB

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKISHO la Serikali za Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu (TAHLISO), limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusikia kilio cha Watanzania na kuahidi kutatua kero ya tozo za miamala.

Vilevile, shirikilisho hilo limemwomba Rais kusaidia upatikanaji wa fedha za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao sasa wanatakiwa kwenda kujifunza kwa vitendo.

Mwenyekiti wa TAHLISO, Frank Nkinda, aliwasilisha maombi yao hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam.

Alisema kuna haja Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kutoa fedha kwa wanafunzi wanaopaswa kwenda masomo ya vitendo.

Alisema tangu wiki iliyopita, baadhi ya wanafunzi wameanza kwenda kujifunza kwa vitendo lakini bado hawajapewa fedha za kujikimu na HESLB.

"Tunaomba Rais Samia atusaidie fedha hizi zitoke mapema ili wanafunzi waweze kwenda 'field' kwa wakati," alisema Nkinda.

Alimshukuru Rais Samia kwa kuona umuhimu wa wanafunzi kuendelea kupata mikopo kwa kuongeza kiwango kutoka Sh. milioni 464 hadi Sh. bilioni 570.

Pia aliishukuru serikali kwa kuondoa riba ya asilimia sita kwenye mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

"Kwa bahati nzuri Rais amesikia kilio chetu kwa kuondoa tozo hii kwa sababu ilikuwa ni mwiba kwa wahitimu wa elimu ya vyuo vikuuu nchini," alisema Nkinda.

Alisema maagizo yaliyotolewa na Rais Samia yanatosha kumshukuru kwa kusikia kilio cha Watanzania wengi ambao wameumizwa na tozo hizo zilizoanza kukatwa hivi karibuni.

Kuhusu tozo za simu, kiongozi huyo alimpongeza Rais kwa kusikia kilio hicho kwa sababu kilikuwa na athari hadi kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Akizungumzia tatizo la uhaba wa ajira kwa wahitimu wa elimu ya juu nchini, alisema serikali imekuwa ikijitahidi kutatua lakini wanafunzi nao wanapaswa kulisaidia taifa kutatua kero zinazolikabili. Alisema serikali imejenga miundombinu kuwawezesha wanafunzi kupata elimu lakini bado wasomi na vijana wa taifa hawajaweza kutafuta mbinu za kutatua shida ya ajira.

Kamishna wa Watu Wenye Mahitaji Maalum wa TAHLISO, Abdallah Abdallah, aliwataka vijana kutengeneza majukwaa mbalimbali ya kuzungumzia kero zao na kuzitatua. Alisema vyuoni kuna kero za miundombinu kwa watu wenye uhitaji maalum, hivyo mazingira yaboreshwe ili wenye uhitaji wapate huduma.

Abdallah pia aliikumbusha serikali kuzingatia Sera ya Ajira kwa watu wenye ulemavu, inayoagiza asilimia tatu ya wanaoajiriwa wawe wenye uhitaji maalum.

Katibu wa TAHLISO, Janet Odillo, aliwataka wanafunzi wanaokutana na vikwazo vya kushindwa kujaza fomu za kuomba mikopo, wafike katika ofisi za serikali za wanafunzi katika vyuo mbalimbali nchini ili waelekezwe namna ya kujaza.

HABARI KITAIFA

## Wanafunzi kortini madai kuchoma maabara, darasa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WANAFUNZI 7 wa Shule ya Sekondari Geita wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Geita kwa makosa mawili ya kuchoma moto maabara na darasa.

Mali hizo zina thamani ya Sh, 153,574,640, na kwamba kitendo hicho ni kinyume cha sheria kifungu cha 319 cha kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019.

Washtakiwa hao ni Henry Benedict (18), Frank Joseph (18), David Samweli (18) na Daudi Magembe (18). Washtakiwa watatu majina yao yanahifadhiwa kutokana na umri wao kuwa mdogo.

Walifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Sosthenes Kiiza, na waliposomewa mashtaka walikana, hivyo kubakia mahabusu kwa kukosa dhamana.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Serikali, Clemence Kato ulidai upelelezi wa kesi hiyo yenye namba 21/2021 haujakamilika, na kuiomba mahakama tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Kiiza alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Agosti 2, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Kiiza aliyataja masharti ya dhamana ni kila mshtakiwa awe na mdhamini mmoja mwenye hati ya nyumba au Sh milion 11.

Hata hivvo, wadhamini wa washtakiwa walishindwa kukidhi masharti, hivyo washtakiwa walipelekwa mahabusu katika gereza la Geita hadi watakapokidhi masharti ya dhamana.

Akisoma hati ya Mashtaka jana Wakili Kato alidai Julai 5, mwaka huu majira ya usiku katika eneo la Shule ya Sekondari Geita, washtakiwa kwa makusudi walichoma moto jengo la darasa la mchepuo wa masomo ya EGM lenye thamani ya Sh. 61,905,120.

Aliendelea kudai kosa la pili ni Julai 6 mwaka huu majira ya usiku katika eneo la shule, ambapo washtakiwa kwa makusudi walichoma moto maabara yenye thamani ya Sh. 91,669,520.

# 5,429 wanaswa madai ya uhalifu kwa miezi 2

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi limesema kwa kipindi cha miezi miwili ya Mei na Juni limekamata wahalifu waliohusika katika kutenda uhalifu wa aina mbalimbali wapatao 5,429.

Jeshi hilo limesema watuhumiwa hao wamekamatwa kutokana na misako, operesheni endelevu na ushirikiano kutoka kwa wananchi.

Hayo yalibainishwa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, David Misime, na kueleza kuwa waliokamatwa kwa kujihusisha na mauaji ni 275, kati yao waliokamatwa kutokana na mauaji ya wivu wa kimapenzi ni 21, imani za kishirikina ni 23 na 231 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kujitafutia kipato kwa njia za kiuhalifu.

Misime alisema waliokamatwa kwa unyang'anyi wa kutumia silaha ni 63, unyang'anyi wa kutumia nguvu (141), kuvunja nyumba na kuiba miwili (1,265), kubaka (508) na kulawiti (125).

Alisema waliokamatwa kwa kujihusisha na makosa ya dawa za kulevya ni 2,300, ambapo Heroin kiasi cha kilo 540 zilikamatwa, cocaine gram 104, bangi kilo 3304.321, mashamba ya bangi hekari 11.75 ziliharibiwa na mirungi kilo 2233.394 zilikamatwa.

Waliokamtwa kwa tuhuma za kujihusisha na utengenezaji wa gongo na kuuza ni 398, na kwamba kiasi kilichokamatwa ni lita 13612.175 na mitambo ya kutengenezea pombe hiyo 94.

Wamo pia waganga wapiga ramri chonganishi ambao alisema ni 15, na kwamba waliokamatwa kulingana na ushahidi ulivyowagusa wameshafikishwa mahakamani.

"Jeshi la Polisi linaendelea kuwasihi wananchi kuendelea kushirikiana nalo ili kupata mafanikio zaidi katika operesheni zinazoendelea ili nchi yetu iendelee kuwa ya amani na utulivu," alisema Misime.

Alisema Jeshi la Polisi katika kila mkoa na kikosi limejipanga vizuri kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama inakuwa shwari wakati wa waumini wa dini ya Kiislamu Tanzania wakiungana na waumini wenzao duniani kusheherekea sikukuu ya Eid Al-Adha.

"Tunatoa wito na karipio kali kwa wahalifu kuachana na vitendo vya kiuhalifu na pia wanaondelea kuwashawishi wananchi kujiingiza kwenye vitendo vya ukiukwaji wa sheria za nchi."



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (wa pili kushoto), akipata maelezo ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Mlandizi-Chalinze-Mboga Chalinze, mkoani Pwani, unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kutoka kwa

# Auawa kwa risasi madai kupora simu

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limemuua kwa kumpiga risasi mwanamume mmoja kwa madai ya kupora simu ya mwanamke.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, Ramadhan Kingai, alithibitisha kuuawa kwa mtuhumiwa huyo aliyedai ni wa ujambazi ambaye alikuwa na mwenzake kwenye pikipiki wakiwa na silaha.

Kamanda Kingai alisema mtuhumiwa huyo aliyeuawa wakiwa kwenye pikipiki, inadaiwa walimpora simu mwanamke katikati ya mtaa wa Tunisia na barabara ya Ali Hassan Mwinyi.

"Bahati nzuri eneo hilo kulikuwa na askari. Baada ya huyo mama kupiga kelele sana, askari walishuhudia wakaanza kuifukuzia pikipiki na mwishowe walipiga risasi juu kutishia askari wasiwafuate. Lakini askari wetu walipiga kuwaelekeza bahati nzuri mmoja akapatikana mmoja akatukimbia," alisema.

Alipoulizwa kuhusu eneo la tukio kupatikana risasi nyingi, Kamanda huyo alisema hizo zinajumuisha risasi za mtuhumiwa wa jambazi na za polisi.

"Baada ya watu hawa kuona wanafuatiliwa na polisi, mtuhumiwa aliyekuwa na silaha akiwa nyuma ya pikipiki alipiga risasi na polisi walijibu. Ujambazi unautofautishaje na ukibaka, kama mtu anakwenda eneo la tukio bunduki huyo ni kibaka au jambazi? Huyu ni jambazi," alisema.

Kamanda Kingai alisema aliyeuawa alikuwa nyuma ya pikipiki ambaye alikuwa akirusha risasi na dereva ambaye alipora simu hawakufanikiwa kumpata.

"Aliyekuwa anapiga risasi ndiye huyu tuliyempata, alidondoka kwenye pikipiki, yule aliyepora simu hatujampata," alisema.

Shuhuda wa tukio hilo, Anania Kidifo, akizungumza na chombo kimoja cha habari (siyo Nipashe), alisema wakati tukio linatokea alikuwa maeneo hayo.

"Wakati tukio linatokea pale, tulianza kusikia milio ya risasi, wakati tunageuka kuangalia ndiyo tukakuta kuna mtu anashambuliwa kwa risasi akawa amelala chini inasemekana alikuwa ni jambazi, askari inaonekana walikuwa eneo hili wamelitanda.

"Kuna askari wengine walitokea upande wa Dar Free Market na wengine walitokea upande wa Leaders kwa hiyo yule mtu wakawa wamemweka kati. Wakati wanamshambulia wale askari waliokuwa upande wa Dar Free Market tukawaambia msiende huko si mnasikia milio ya risasi.

"Wakasema wapo kazini tukawaacha wakavuka kuelekea eneo la tukio, zilipigwa risasi nyingi sana karibu 40, ilikuwa milio ya risasi kama tupo uwanja wa vita," alisema.

Shuhuda huyo alisema baadaye mmoja wa askari aliyevalia sare alikwenda eneo la tukio na wao walisogea kushuhudia.

"Tulishuhudia yule mtu aliyekuwa amelala chini amemiminiwa risasi nyingi za kutosha wakati wanampekua wakakuta ana bastola huku akiwa amelala chini ameshakufa," alisema.

"Inasemekana mtu huyu alikuwa amesimama hapo peke yake alikuwa na pikipiki aina ya boxer mpya na wakati akishambuliwa inadaiwa alikuwa amesimama hapo hapo," alisimulia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 981 kupata mimba Kibondo tishio kwa ustawi wa mtoto wa kike

**JUMLA** ya wanafunzi 981 wilayani Kibondo, mkoani Kigoma walipata mimba katika kipindi cha miezi sita, Januari hadi Juni, mwaka huu, sasa wako nyumbani wamekosa haki yao ya kupata elimu.

Takwimu hizo ni wastani wa wanafunzi 163 kila mwezi na mwezi na mwezi mmoja ulikuwa na wanafunzi 164, mwezi mwingine 165 ambao waliacha masomo kwa sababu ya kupata mimba. Takwimu hizo ni kwa waliopata mimba bado za utoro ambao uhusisha wanafunzi wa kike na kiume hazijatajwa, na hii ni kwa wilaya moja kwamba ndoto za wanafunzi hawa zimekufa kwa kulazimishwa, kulaghaiwa au kwa uwezo mdogo wa kuchambua mambo na kujikuta kwenye mitego wa waharibifu.

Hali hii siyo ya kuridhisha kwa kuwa inaongeza idadi ya wajinga kwenye jamii ambao sasa watazaa watoto ambao huenda wakapita njia hiyo hiyo, mama hakusoma na mtoto naye hatasoma maana yake inaandaliwa jamii isiyoelimika ambayo ni ngumu kufanya uamuzi au kuchangia uchumi wa nchi bali kuendelea kuzalisha wategemezi. Ujinga ni mzigo wa taifa na ndiyo maana zimekuja shule ili watu wasome na kuelimika kwa namna tofauti, ikiwamo kujua kusoma na kuandika ili kumudu maisha kwa kuwa yanahitaji watu walioelimika. Jambo hili lina sura nyingi mojawapo ni wazazi au walezi kushindwa kufuatilia kwa karibu maendeleo ya watoto wao, kwa kuwa inaonekana wanajilea wenyewe. Mifano ni mingi ambayo inaonyesha wapo watoto wanajilea wenyewe, na wakati mwingine wazazi wanawageuza watoto mtaji wa kujipatia kipato kiasi cha baadhi kujihusisha na mambo yasiyostahili. Ni wajibu wa wazazi, walezi na serikali kushirikiana kukomesha tabia hii, inawezekana hao wamefahamika, lakini kuna idadi kubwa ambao hawajafahamika na waliacha shule wanalea watoto, mtoto analea mtoto mwenzake. Yawezekana kuna ambao wako shuleni na wana ujauzito, lakini kwa kuwa bado hawajapimwa ni rahisi kujificha na kuacha shule au kuendelea na masomo kwa kuwa maumbile hutofautiana. Hatari nyingine ni za kiafya kwamba kwa umri wa chini ya miaka 18 kujifungua ni kwa tabu na kuna uwezekano wa kupoteza maisha, huku wengine wakipata fistula na maradhi mengine yanayosababishwa na uzazi katika umri mdogo.

Sheria ya elimu imeweka wazi adhabu inayotolewa kwa mtu anayebainika kumpa ujauzito mwanafunzi ni kifungo cha miaka 30 jela, ni lazima hatua zichukuliwe ili iwe fundisho kwa wengine wanaotamani kuwa kwenye mahusiano na wanafunzi.

Ifike mahali jambo hili lizungumzwe kama agenda muhimu kwenye mikutano ya hadhara ya kijiji ambayo hujumuisha wenyeviti wa vitongoji vyote na wananchi, na kamati ya ushauri ya kata (WDC) ambayo mwenyekiti wake ni diwani wa kata na wajumbe ni wenyeviti wa vijiji huku mtendaji wa kata akiwa katibu na baadaye kwenye Baraza la Madiwani ambalo huundwa na madiwani wa kata zote za wilaya au eneo la utawala la halmashauri ambao huchagua Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji huwa Katibu wa kikao na wajumbe wengine ni wakuu wa idara za halmasahuri husika, ili ijulikane na hatua zichukuliwe kuhakikisha kizazi cha baadaye kinaokolewa. Kukiwa na ushirikiano baina ya serikali na wadau wote kuna uwezekano mkubwa wa kushughulikia tatizo hilo, ikiwamo kuja na mkakati maalum wa kuwaendeleza wanafunzi hawa ambao haki yao ya kusoma imekatishwa kwa kulaghaiwa, kukubali wenyewe au kubakwa.

Jitihada nyingi zinafanyika kuongeza idadi ya wanawake waliosoma, kwenye ngazi za uamuzi na nguvu ya kiuchumi, sasa kinapotokea kikwazo kama hiki maana yake idadi ya wanawake waliosoma inapungua, wenye nguvu ya kiuchumi na wanaoweza kushika madaraka katika uamuzi mbalimbali. Miongoni mwa wanafunzi hao 981 wapo madaktari, wabunge, mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa mkoa na wilaya na wakurugenzi watendaji wa halmashauri mbalimbali, lakini kwasababu ya ujauzito wameshindwa kuendelea na masomo yao kama watoto wengine.





## Muungwana Lazima Nilonge

# Waandishi wanawake wanasahaulika kiajira

Na Zainabu Ramadhani, SJMC

**UANDISHI** wa habari ni moja ya fani muhimu kwenye jamii kwani ni daraja linalounganisha na kufikisha taarifa kutoka kwa watoaji na kuwapelekea wananchi.

Jukumu hilo ni nyeti kutokana na ulazima wa binadamu kuhabarika na taarifa muhimu na za mara kwa mara katika mazingira na dunia anayoishi.

Dhana hii ya upashanaji habari ni ya karne nyingi kwa vile ilianza kwa kutumia michoro na picha zilizochorwa mapangoni na hata kwenye mawe ili kufikisha ujumbe kwa jamii ama kundi fulani.

Na hilo lilidumu kwa miongo mingi kutoka kizazi kimoja hadi vingine hadi ujio wa sayansi na teknolojia ulioboresha mawasiliano kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kutokana na umuhimu huo ndiyo maana miaka ya hivi karibuni kumekuwa mabadiliko makubwa katika tasnia ya uandishi na usambazaji wa habari yanayoletwa na TEHAMA.

Yote hayo yamechangia kuongezeka kwa idadi kubwa ya wanaume na wanawake kwenye tasnia hiyo. Na wote hao wamejikita katika kutafuta maarifa na taaluma ili kuifikishia jamii taarifa sahihi na kwa wakati kwa kutumia ujuzi walioupata madarasani na teknolojia wezeshi.

Katika safari ya kutafuta taaluma hii ya uandishi wa habari, kumezuka changamoto kubwa ya upatikanaji wa ajira rasmi kwa wahitimu hasa kwa wanawake.

Mathalani, baadhi wameijikuta wakiingizwa kwenye mahangaiko makubwa ili wapate ajira mahali fulani walipo patamani. Hili limechangia kushusha morali yao ya kuthamini kile walichojifunza wakiwa darasani na umuhimu wake kwa jamii.

Lakini, wanawake wanazidi kukata tamaa kwa vile wengi hawaaminiki katika tasnia hiyo na kuwaona kama watu wa ajabu hasa wakishika kamera na kazi nyingine ambazo zimezoeleka kuwa ni za wanaume. Kimazoea wanawake walikuwa wakihusishwa na usomaji wa habari na siyo vitengo vingine.

Na hili mara nyingi limekuwa likiathiri taaluma yao kwasababu ya kupangiwa nini cha kufanya na kile cha kutokugusa.

Zaidi waandishi wa habari wa kike wamejikuta wakiathirika na ukosefu wa ajira na kuangukia kwenye kufanya majukumu mengine ambazo si za taaluma hiyo.

Mbali na hayo ukosefu wa ajira kwa wasichana waandishi umefanya fani hiyo kuathirika kwa kukosa wanafunzi wapya, kwani wengi wao wamekuwa wakikataa kujiunga kwa kisingizo cha kuepuka kusota bila ajira kama ilivyo kwa watangulizi wao. Hali hii pia inachangia waandishi kutothaminiwa wala kupewa kipaumbele kama zilivo kazi nyingine, na upatikanaji wake wa ajira kuwa mgumu hususani kwa wanawake na kutokana na imani zilizojengeka katika jamii kuwa uandishi wa habari soko lake la ajira limekuwa dogo likilinganishwa na sekta nyingine

Wanahabari waathirika wanaiomba serikali na asasi binafsi, kupanua wigo wa ajira ili wasichana waandishi waongezeke kwenye fani hii muhimu.

Pia taasisi nyingine za fedha ziwe tayari kuweka mazingira bora ya kutoa mikopo nafuu kwa vijana na hasa waandishi wa habari wa kike ili kuwawezesha kuanzisha kampuni zao binafsi na kujiajiri kusaidia kujikwamua na pia kuajiri wengine.

Ni raia yangu kwa waandishi wanafunzi walio kwenye mafunzo au wanaotarajia kwenda kwenye mafunzo kwa vitendo kujiepusha na tabia zinazoharibu maadili yao na kujidhalilisha ili kuweka mazingira ya kuajiriwa baadae

Ninalisitiza hili kwasababu chanzo cha kushamiri tatizo la ukosefu wa ajira kwa waandishi wengi wa kike ni matokeo ya kujifunga katika mienendo isiyo ya kimaadili na kusababisha wasiajirike.

Naamini kwa kupitia makala hii, wahusika wote wataliangalia kwa jicho la karibu tatizo hili la ukosefu wa ajira kwa waandishi wa habari wa kike na kuja na muarobaini wa kulimaliza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

# HABARI KITAIFA

## Mtoto afariki dunia machimbo mchanga

**Na Mary Geofrey**

MWANAFUNZI wa darasa la kwanza katika Shule ya Msingi Bunju B, Gift Athumani (9), amefariki dunia baada ya kudaiwa kutumbukia kwenye shimo la mchanga.

Tukio hilo lilitokea juzi Mto Mpiji, eneo la Uwanja wa Simba, Kiyonzile, Kata ya Bunju B wilayani Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Jirani wa mtoto huyo, Miriam Kiwawa, aliliambia Nipashe jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa tisa alasiri wakati mtoto huyo alipokwenda na mwenzake mtoni kwa lengo la kuchota maji.

Alisema mtoto huyo alitoka shuleni mchana kurejea nyumbani na baada ya muda, alitoka na mtoto mwenzie kwa lengo la kwenda kuchota maji.

Alisema mtoto huyo alifika na kusogea ndani ya maji ili ayateke lakini kwa bahati mbaya kulikuwa na shimo ndipo akaanza kutitia.

"Yule mtoto mwingine alipoona mwenzake amezama, alikimbia kwenda kutoa taarifa kwa majirani ambao walikimbia na kufika mtoni wakakuta mtoto huyo alishazama," alisema Aloyce Joseph, mmoja wa majirani.

Alisema walitafutwa vijana ambao waliingia ndani ya maji na kumtoa ambako alikuwa amenasa chini kwenye tope.

"Alitolewa akiwa ameshafariki dunia kwa sababu tukio hilo lilichukua muda mrefu kidogo hadi watoto kutoa taarifa hadi kuokolewa.

"Hili tukio ni la tatu kutokea katika mto huu, yalishatokea mengine mawili, watoto wengine wawili walikufa kama alivyokufa huyu mtoto, tunaiomba serikali iangalie namna ya kudhibiti uchimbaji huu wa mchanga," alisema.

Alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo walitoa taarifa katika Kituo cha Polisi Magwepande.

Mwenyekiti wa Baraka la Wazee wa Shina Na. 11 la Uwanja wa Simba, Simon Mpina, pia aliiomba serikali kuzuia uchimbaji mchanga katika eneo hilo.

Alisema eneo alilotumbukia mtoto huyo ni umbali wa mita 150 hadi kwenye makazi ya watu, hivyo ni rahisi watoto wengine kuendelea kupoteza maisha bila kuokolewa.

Alisema mwili wa mtoto huyo, umehifadhiwa katika Hospitali ya Kerege na kwamba maziko yanatarajiwa kufanyika leo katika makaburi ya eneo la soko jipya la Bunju B.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Hassan Mnondwa, alikiri kutokea kwa tukio, akikiri uchimbaji wa mchanga katika mto huyo umekuwa tatizo kubwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Ramadhan Kingai, alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia tukio hilo jana, alisema hakuwa na taarifa hizo, lakini akaahidi kufuatilia.



Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Biashara ya DCB, Zacharia Kapama (kushoto), akizungumza na wanahisa wa benki hiyo wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam jana. Kutoka kushoto kwake ni Mweka Hazina wa Jiji hilo, Tulusubya Kamalamo, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji hilo, Tabu Shaibu, Mkurugenzi Mtendaji wa DCB, Godfrey Ndalahwa, Mstahiki Meya wa Jiji, Omari Kumbilamoto na Naibu Meya, Saady Khimji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NBAA yaonya kampuni kukwepa ukaguzi

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), imesema haitasita kuwafutia usajili kampuni za ukaguzi wa hesabu ambazo zitabainika kukwepa kukaguliwa na bodi hiyo.

Kwa mujibu wa NBAA, ziko baadhi ya kampuni ambazo zimekuwa zikikwepa kukaguliwa na wakati mwingine kushindwa kutoa ushirikiano mzuri wakati maofisa kutoka katika bodi hiyo wanapowatembelea kwa ajili ya kukagua ubora wa viwango vya kaguzi zao.

Ofisa Mdhibiti wa Viwango wa NBAA, Winnington Makaka, alisema hayo jijini Dar es Salaam, na kwamba hali hiyo siyo tu kwamba inakwamisha kazi za bodi hiyo, bali pia inaathiri zaidi taaluma ya ukaguzi na uhasibu kwa ujumla.

"Mara nyingi tumekuwa tukikabiliwa na vizuizi tunapofanya kazi za ukaguzi kwenye kampuni hizi, ni vema zikatambua kwamba hiki tunachokifanya ni sharti la kisheria, hivyo zinapaswa kutambua kuwa kuwazuia maofisa wa NBAA kutekeleza majukumu yao ni kinyume cha sheria na inaweza kuchangia kufungwa kwa kampuni zao," alisema Makaka.

"Tunatoa wito kwa kampuni zote za ukaguzi, kuhakikisha kuwa zinatii viwango vya ukaguzi vilivyowekwa ikiwa ni pamoja na kuwa na maadili, kupitia taarifa za kifedha za mashirika mbalimbali na kutoa ushirikiano kwa NBAA."

Ofisa Masoko wa NBAA, Magreth Kageya, alisema wahasibu na wakaguzi wana nafasi kubwa katika jamii na kwamba kuna haja ya wao kuhakikisha wanalinda maadili yao kwa kiwango cha juu ili umma uendelee kuwa na imani nao.

Kageya aliwataka wahasibu na wakaguzi hao kuhakikisha wanaheshimu na kulinda viapo vyao vya kitaaluma wanapotekeleza majukumu yao.

Alisema Bodi imetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya taaluma ya uhasibu nchini kwa miaka mingi, na kwamba itahakikisha inaendelea kutoa michango yake katika kuendelea kuiimarisha zaidi taaluma hiyo.

## Waziri azipa kibarua halmashauri

**Na Munir Shemweta,**
SUMBAWANGA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezitaka halmashauri nchini kutoa hati zisizopungua 100 kila moja kwa mwezi.

Akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi katika Mkoa wa Rukwa juzi, akiwa katika ziara ya kukagua utendaji kazi sekta ya ardhi nchini, Dk. Mabula alisema halmashauri kupitia idara zao za ardhi zinatakiwa kuandaa hati zisizopungua 100 kwa mwezi katika maeneo ambayo viwanja vimepimwa.

"Kule ambako viwanja havijapimwa, watendaji wake wanaweza kueleweka lakini mtu ana viwanja 100 halafu anashindwa hati za idadi hiyo na wakati mwingine anatoa hati 10 tu huku akiwa amejiwekea lengo la kutoa hati 100," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, hatimiliki za ardhi zisipotoka na kupewa wamiliki wa ardhi, migogoro haitaisha na matokeo yake ni kuwapo umilikishaji mara mbili.

Alimtaka Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Rukwa, Swagile Mfinanga, kumpatia taarifa ya uandaaji hati kwa kila halmashauri yake kufikia mwisho wa Agosti, mwaka huu.

Pia alisisitiza kuwa hatua hiyo pia itafika mikoa yote kwa kuangalia idadi ya viwanja vilivyopimwa na wamiliki wangapi wameomba lakini hawajapatiwa na kama hawajaomba mara ngapi watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri husika wamekwenda kuhamasisha ili wamiliki waombe kupatiwa hati.

Katika hatua nyingine, Dk. Mabula aligawa ankara za malipo ya kumilikishwa ardhi kwa wananchi 593 waliopimiwa maeneo yao katika kata ya Momoka, Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa.

Naibu Waziri aliwaambia wakazi hao kuwa wamefanya jambo zuri la kukubali kupimiwa maeneo yao ili baadaye kumilikishwa na wizara inawaunga mkono kwa kuwa uamuzi waliofanya utawasaidia kuepukana na migogoro ya mipaka na wakati huo huo kutumia hati watakazopata katika shughuli za maendeleo kama vile kuchukulia mikopo benki.

# Benki yatoa bima kwa wakulima 700

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

BENKI ya Azania kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku Wilaya ya Chunya, (CHUTCU), wametiliana saini makubaliano ya kuwawezesha wakulima wa zao hilo kujiunga na bima afya ili kupata matibabu bure.

Makubaliano hayo yalifanyika juzi baina ya taasisi hizo katika kata ya Lupa Tingatinga, Chunya mkoani Mbeya na kushuhudiwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon.

Akizungumza katika hafla hiyo, Meneja Mwandamizi wa Biashara wa Azania Bank, Jackson Lohay, alisema katika makubaliano hayo, benki hiyo itatoa mkopo usiokuwa na riba kwa ajili ya kuwawezesha zaidi ya wakulima 700 kupata bima ya afya.

"Katika mkataba wetu tutawawezesha wanachama ambao wako chini ya chama kikuu cha ushirika ambao ni zaidi ya 700 lakini watakaonufaika na mpango ni zaidi ya watu 2,000 wanaotegemewa na wanachama," alisema

Lohay alisema fedha hizo zitarejeshwa baada ya wakulima kuvuna mazao yao na kuyauza.

Mpango wa bima kwa wakulima umebuniwa baada ya kuona fedha nyingi za wakulima zinaishia kwenye kilimo, hivyo kushindwa kuwekeza kwenye afya zao hali inayosababisha kuuza rasilimali zao ili wapate gharama za matibabu wanapopatwa na maradhi.

"Ugonjwa haupigi hodi ndugu zangu. Hatua hii pia ni ukombozi kwa wakulima wengi, ambao huilisha nchi, kuingia kwenye mfumo wa bima baada ya kuwa nje ya mfumo kwa muda mrefu," alisisitiza.

Kampuni nyingi za huduma za bima zimekuwa zikikwepa kuwapa bima wakulima kwa madai kuwa biashara zao hazitabiriki.

Meneja wa NHIF Mkoa wa Mbeya, Mbala Shitindi, alisema mpango huo utaondoa kikwazo cha wakulima kushindwa kupata huduma za matibabu kutokana na kuwa na kipato kidogo.

Aliwasihi wakulima kutumia fursa ya kupata mkopo huo ambao hauna riba kujiunga na bima ya afya kwa kuwa suala la afya ndilo mtaji wao wa kufanya shughuli za uzalishaji kupitia sekta ya kilimo.

"Huo si mkopo ni fedha ambazo mmeazimwa tu kwa kuwa hauna riba. Naamini itasaidia kuondoa changamoto kwa kuwa wakulima wengi tulikuwa tunashindwa kugharamia Sh. 76,800 za matibabu kwa mwaka," alisema.

Kwa upande wake, Mayeka aliishukuru Azania Bank kwa kuamua kuwakopesha wakulima fedha za bima ya afya bila riba na kwamba hatua hiyo inaunga mkono maono ya serikali kuhakikisha wananchi wote wanajiunga na bima ya afya.

"Afya ndiyo msingi wa kila kitu. Kama huna uhakika wa afya yako hakuna haja ya kupangilia mipango ya mbele na niwaambie tunakoelekea mfumo wa kutibiwa kwa 'cash' (fedha tasilimu) utaondolewa, hivyo ni vyema wananchi wote tuanze kufikiria kujiunga na bima," alisema.

Baadhi ya wakulima ambao watanufaika na mkopo huo walisema bima hiyo itawawezesha kuwa na uhakika wa kupata matibabu bure wao na familia zao.

"Tumepokea kwa furaha mkopo huo na umekuja kwa wakati mwafaka kwani utatuwezesha sisi na familia zetu kupata matibabu bure hata kama hatuna fedha kwa wakati huo," alisema Grace Mpigauzi, mkazi wa Lupa Tingatinga.

Hatua hii ni muhimu sana kwa serikali kupitia Mamlaka ya usimamizi wa shughuli za bima (TIRA) katika kutimiza lengo la kutoa elimu ya Bima kwa asilimia 80 ya Watanzania kufikia mwaka 2030, kutoka asilimia 36 ya sasa.

Pia kuongeza idadi ya watumiaji wa bima, kutoka asilimia 15 ya sasa mpaka asilimia 50 mwaka 2030.




Meneja mwandamizi wa biashara kutoka Benki ya Azania, Jackson Lohay (kulia), akikabidhiana nyaraka za mkataba wa mkopo wa bima ya afya na Makamu Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha wilaya ya Chunya (CHUTCU), Elieza Fijadh (katikati), jijini Mbeya jana. Kushoto ni Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoa wa Mbeya, Mbala Shitindi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NHC yawekeza bil. 7.3/- Katavi

**Na Munir Shemweta,** KATAVI

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limewekeza Sh. bilioni 7.3 katika Mkoa wa Katavi baada ya kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi katika mkoa huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi wa nyumba za makazi Inyonga uliofanywa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, juzi, Meneja wa NHC mikoa ya Rukwa na Katavi, Mhandisi Patrick Kamendu, alisema miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ile nyumba za makazi katika maeneo ya Ilembo, Inyonga, Kakuni na jengo la Kitega Uchumi la Mpanda Plaza.

Pamoja na uwekezaji huo, alisema NHC imejenga kama Mkandarasi Jengo la Ofisi la Wakala wa Misitu Tanzania(TFS) lililogharimu Sh. milioni 263 ambalo alisema limekamilika na limekabidhiwa kwa wahusika. Dk. Mabula aliipongeza NHC kwa kufanikisha kutekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba za makazi kwenye mkoa huo wa Katavi kwa ufanisi na kuitaka kuongeza kasi ya ujenzi ya miradi katika eneo la Inyonga palipojengwa nyumba za makazi ili kukidhi kiu ya wananchi wanaohitaji nyumba za kuishi.

"Nawasihi muongeze kasi ya ujenzi wa nyumba za makazi katika maeneo haya kwani uhitaji ni mkubwa ili Mlele pavutie na watu waendelee kwenda kuishi," alisema. Kwa mujibu wa Kamendu, Inyonga palipojengwa nyumba za makazi ni eneo la viwanja 70 vilivyonunuliwa na shirika kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mlele. Pia alisema kuna viwanja vilivyobaki alivyovisema vitaendelezwa baadaye. Meneja huyo alibainisha kuwa mradi huo umetekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele na kuwekewa jiwe la msingi na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahaman Kinana.

Kamendu alisema mradi huo una nyumba 24 za makazi na ulianza kutekelezwa Juni, 2014 kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato ya shirika.

Hadi kukamilika, mradi wa nyumba wa Inyonga umegharamu Sh. 991,482,480 ambazo ni fedha za mapato ya ndani ya shirika ambazo zinazotumika kuongeza mapato ya mikoa midogo na kuhakikisha huduma za shirika zinafika katika mikoa yote nchini.

# Hatua zaanza kukabili makali bei ya mbolea

**Na Enock Charles**

SERIKALI imesema inatarajia bei ya mbolea kushuka katika siku chache zijazo, kutokana na shehena za mbolea takriban tani 25,000 kuanza kuingia kwa wingi nchini kuanzia mwezi huu.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza akiwa bandarini Dar es Salaam jana, alisema kupanda bei kwa bidhaa hiyo kulitokana na uhitaji mkubwa wa mbolea katika nchi nyingi duniani kulikosababisha kupanda kwa bidhaa hiyo katika soko la dunia.

"Mbolea ilipanda kutokana na demand (uhitaji) wa bidhaa katika mataifa mbalimbali duniani, kwa hiyo baada ya nchi hizo kununua na kuanza kuitumia mbolea itakuwa na unafuu kwa sababu gharama ya uzalishaji wa mbolea haijapanda sana," alisema Prof. Mkenda.

"Mimi kwa mfano nimetembelea kiwanda cha phosphate kule Morocco, gharama ziko pale pale kilichoongezeka ni wanunuzi wananunua kwa wingi... kwa hiyo bei ikapanda na wale wanunuzi mpaka mwezi wa nane hivi kati kati tunaamini watakuwa wameshachukua shehena wanayohitaji, hivyo bei itashuka,"aliongeza.

Alisema kutokana na kuingia kwa wingi kwa mbolea, ambayo waagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi wameshaagiza, na kuondolewa kwa urasimu wa uagizaji katika mfumo wa uagizaji wa pamoja na kuruhusiwa kila mwenye uwezo kuagiza mwenyewe, ni matarajio ya Serikali kuwa bidhaa hiyo sasa itashuka bei kuliko ilivyo sasa. Akizungumzia shehena za mbolea zinazotarajiwa kuingia, Kaimu Meneja wa Sehemu ya Kichele bandarini hapo inayohusika na bidhaa za kichele kama mbolea, Tatu Moyo, alisema wanatarajia kupokea tani 11,000 ya mbolea aina ya granula, Jumapili kutoka kampuni ya ETG , Julai 29, mwaka huu tani 4,753 ya mbolea aina ya granula , Julai 31mwaka huu tani 9,400 ya mbolea aina ya CAN.

Akizungumza na waagizaji na wasafirishaji wa mbolea mwishoni mwa wiki , Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema Wizara hiyo ina mpango wa kuzungumza na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili kupunguza bei za usafirishaji wa bidhaa hiyo kutoka kwa wafanyabiashara kwenda maeneo mbalimbali ya nchi.

## Mbolea ya kilimo hai yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

MBOLEA ya asili inayojulikana kwa jina Hakika imezinduliwa ili kukuza aina ya kilimo kinachoitwa kilimohai (organic farming) kwa ajili ya kupanua soko la mazao yanayotokana na kilimo hicho.

Lengo lingine ni kuimarisha afya ya udongo na kuongeza tija katika kilimo cha wanavijiji.

Mbole hiyo inatengenezwa na Kampuni ya Kitanzania ya Guavay ambapo Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Mhandisi Ahad Katera, alisema kwamba kampuni inafanya jitihada ya kuongeza uzalishaji kutoka tani 3,500 za sasa hadi tani 20,000 kwa mwaka.

"Lengo letu ni kuhakikisha wakulima wa parachichi nchini wanayafikia masoko ya Ulaya na Marekani kwa njia ya uzalishaji wenye tija na matunda yao kukubalika katika masoko hayo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kisa Kasongwa, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Mhandishi Marwa Rubirya, aliipongeza Kampuni ya Guavay na wadau wote walioshiriki katika utafiti hadi ikapatikana mbolea hiyo.

## Ruvuma yaunda baraza la wazee

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WAZEE wa Mkoa wa Ruvuma wamefanya kikao maalum cha uundaji Baraza la Wazee la Mkoa kilichofanyika mjini Songea.

Waliochaguliwa kwenye uchaguzi ulioshirikisha wawakilishi kutoka wilaya za Nyasa, Mbinga, Songea, Tunduru na Namtumbo ni Mwenyekiti, Elenzian Nyoni kutoka Manispaa ya Songea.

Wengine ni Lusiana Nduguru kutoka Halmashauri ya Mji wa Mbinga (Makamu Mwenyekiti), Katibu ni Winfrid Mbilinyi kutoka Halmashauri ya Madaba na Naibu Katibu, Philipo Katyale kutoka Halmashauri ya Songea.

Viongozi wengine waliochaguliwa kuunda Baraza la Wazee wa Mkoa ni Mtunza Hazina, Esta Nzuyu kutoka Halmashauri ya Mji wa Mbinga, Mwakilishi wa wanaume, Yustin Mande kutoka Halmashauri ya Nyasa na Mwakilishi wa wanawake amechaguliwa Maria Luoga kutoka Manispaa ya Songea.

Akizungumza wakati anafungua kikao cha uchaguzi huo, mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Bakari Ally Mketo, alisema Taifa linawategemea sana wazee ambao ni hazina kubwa katika jamii.

Alisema serikali imetoa nguvu kubwa katika mabaraza ya wazee, na kwamba busara ya wazee kwenye mabaraza hayo itasaidia kutafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wazee.

# Kamati ya DC kuchunguza ushuru sokoni yaanza kazi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

KAMATI ya wajumbe wanane iliyoundwa na Mkuu wa Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Claudia Kitta, kuchunguza madai ya wafanyabiashara wa soko kuu la Mkuti kubambikiwa fedha za ushuru wa mabanda na halmashauri ya Mji Masasi, imeanza kazi.

Kamati hiyo ilianza kazi juzi ili kujua uhalali wa madai yao, huku Kitta akiipa siku tatu kukamilisha uchunguzi huo kasha kuja na taarifa kamili.

Akizungumza na wafanyabiashara hao kwenye mkutano maalum, Kitta alisema ameamua kuunda kamati hiyo kupata ukweli kuepukana na mgogoro kati ya yao na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Masasi, Gimbana Ntavyo.

Alisema kazi ya kamati hiyo ni kuchunguza na kupitia mpya orodha yote ya wafanyabiashara na kujiridhirisha juu ya kinachoelezwa kwamba wamebambikiziwa madeni ya ushuru ya mabanda ya soko na halmashauri, huku baadhi yao wakieleza kulipishwa ushuru kila mwezi bila ya kupewa risiti na wakusanyaji wa halmashauri kwa zaidi ya miaka mitatu na zaidi.

Mkuu huyo wa wilaya alisema serikali itahakikisha inamaliza mvutano huo kwa haki bila upendo wowote na kwamba kama ikibainika kuna watendaji wa serikali wamefuja fedha za serikali, hatua za kisheria lazima zichukuliwe dhidi yao.

Vilevile, alisema kama wapo wafanyabiashara ambao wanadaiwa, nilazima walipe madeni hayo na wale waliolipa ila wamebambikiziwa madeni, watafutiwa madeni hayo.

Mwenyekiti wa soko hilo, Abdallah Mtandama, alisema wanakubaliana na hatua ya mkuu wa wilaya ya kuunda kamati na kwamba wamebambiziwa madeni kwa sababu wapo waliolipa na kutodaiwa, ila wametajwa kudaiwa na halmashauri, jambo ambalo sio sahihi.



Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na watu wenye uhitaji maalumu, baada ya kuwakabidhi viti mwendo vitatu kwa jijini humo, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wajawazito wapata ahueni huduma za afya

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WAJAWAZITO katika vijiji vitatu katika Halmashauri wa Wilaya Ushetu mkoani Shinyanga, wanajifungulia majumbani kutokana na ukosefu wa huduma za afya.

Wanawake hao wanatoka katika vijiji vya Misayu, Ihata, na Mwadui mkoani Shinyanga.

Walibainisha hayo juzi wakati wadau wa maendeleo kutoka kampuni za ununuzi wa zao la tumbaku kutoa Sh. milioni 464 kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga.

Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na ununuzi wa vifaa tiba katika hafla iliyofanyika kwenye Kijiji cha Misayu.

Mmoja wa wanawake hao, Ester Bundala, alisema wajawazito wengi kwenye vijiji hivyo wanajifungulia majumbani kutokana na ukosefu wa huduma ya afya.

'Tunapojifungulia nyumbani kwa kuzalishwa na wakunga wa jadi huwa tupo katika hatari kubwa ya kupoteza maisha, sababu wao hawana vifaa maalum vya kuhudumia mjamzito hasa pale unapomwaga damu nyingi au kuhitaji kujifungua kwa upasuaji, matokeo yake mzazi anafariki," alisema Bundala. Naye Mariamu Masunga kutoka Kijiji cha Misayu, alipongeza kutolewa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, ambayo itawasogezea huduma karibu.

Naye Meneja mradi kutoka kampuni ya Tambuka, Osca Luoga, alisema ujenzi huo wa zahanati kwenye kijiji hicho cha Misayu, utakuwa msaada kwa vijiji hivyo.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, alisema wataendelea kuzihimiza kampuni zingine za ununuzi wa zao hilo kurudisha sehemu ya faida wanazozipata kwa kuwatatulia wananchi kero mbalimbali ikiwamo sekta ya afya, elimu na maji.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema kampuni hiyo imekuwa na uzalendo kwa kurudisha faida kwa wananchi kutatua kero zao, huku akiwataka wanawake kuacha kujifungulia majumbani ili kupuguza vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi.

# Wanaofanya biashara barabarani wahamishwe, aagiza RC Makalla

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ameiagiza Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam kuwaondoa wafanyabiashara wanaoendesha biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi ikiwamo hifadhi za barabara na kuwatafutia vizimba kwenye masoko.

Akizungumza alipotembelea Soko la Kariakoo, Machinga Complex na Kisutu, alisema ameridhishwa kuona waathirika wa moto Kariakoo wamepata maeneo na kuendelea na biashara zao kama kawaida.

Kuhusu ukarabati wa maeneo walipofikia wafanyabiashara hao, alisema zaidi ya Sh. milioni 62 zitatafutwa ili kukarabati Soko la Machinga Complex na ukarabati huo wa paa la kivuli kwa wauza mboga na matunda utaanza wiki ijayo.

"Katika soko la Kisutu wale waliopewa maeneo ya kujenga fremu waruhusiwe kujenga na wasizungushwe na gharama zao ziwekwe wazi ili waendelee na shuhuli zao," alisisitiza.

Makalla aliahidi wafanyabiashara kuwa mstari wa mbele katika kuwatafutia wateja, huku akisisitiza agizo lake la kutaka wasitozwe ushuru kwa miezi miwili kama sehemu ya kifuta machozi.

Mmoja wa wafanyabiashara walioathirika kwa moto katika Soko la Kariakoo, Radhid Mohamed, aliishukuru serikali na viongozi wa mkoa huo kwa ushirikiano mzuri waliowapatia wakati wa janga hilo.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Mwembesongo, Abdula Omary akizungumza jambo wakati wa kongamano la benki ya NMB na walimu lililofanyika mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ukaguzi bima magari bandarini waanza

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imezindua kituo cha ukaguzi wa bima za vyombo vya moto Bandari ya Dar es Salaam baada ya kubaini magari yanayokwenda nje ya nchi kutokea bandarini hapo baadhi yana bima zisizo halali na mengine hayana.

Uzinduzi ulifanyika katika Bandari ya Dar es Salaam na kushuhudiwa na Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema, pamoja na wadau wa huduma hiyo.

Kamishna wa Bima, Dk. Mussa Juma, alisema kuanzia sasa magari yote yanayokwenda nje ya nchi hayataruhusiwa kutoka bandarini hapo bila ya kuwa na bima.

Alisema kituo hicho ni kwa ajili ya vyombo vya moto mara vinapowasili nchini kwa njia ya meli.

"Kipekee nimshukuru Mkurugenzi Mkuu na uongozi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa kutupa nafasi katika bandari ili tupate fursa ya kutimiza wajibu wa sheria na miongozo mbalimbali.

"Kama mnavyofahamu TIRA ina wajibu mkubwa katika kuhakikisha huduma na biashara ya bima inakuwa mahali pa kukimbilia linapotokea janga, hivyo tuna budi kuweka utaratibu mzuri ili wananchi wahudumiwe."

Dk. Juma alisema kituo hicho kitatumika kukagua bima za vyombo vya moto kabla ya kutoka nje ya geti la bandari na kwamba huduma ya bima zote zitafanyika gari likiwa bandarini.

Alisema ni kosa la kisheria kwa chombo cha moto kutembea bila bima katika ardhi ya Tanzania.

Alisema kwa kawaida magari yanayokwenda nje ya nchi hutoka hadi usiku wa manane wakati wao shughuli zao zinafanyika mchana.

"Tumeona tuwe na kituo hiki tuthibiti ili tupate takwimu sahihi za wiki na mwezi za magari yanayotoka bandarini kwenda nchi mbalimbali, vilevile kumekuwa na upotevu mkubwa wa tozo. Tunaanza na magari yanayokwenda nchi mbalimbali na huko mbeleni tutatoa huduma kwa magari ya ndani," alisema.

Lema aliviagiza vyombo vyote ikiwamo TIRA vitakavyokuwa bandarini hapo vitoe ushirikiano wa kutosha kwa wafanyakazi wa bandari hasa kitengo cha ulinzi ili kuhakikisha haiharibu utaratibu wa utoaji wa magari waliojiwekea.

Alisema lengo walilojiwekea ni kutoa magari yasiyopungua kwa siku kati ya 800 hadi 1,200.

"Ninatarajia kupitia kituo hiki, tutafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha ubora na ufanisi wa Bandari katika kuhudumia utoaji magari unaendelea vizuri bila kuathiriwa," alisema.

Athanas Kikuji kutoka Umoja wa Kampuni za Bima Tanzania, alisema mtu anapokuwa na bima anakuwa na uhakika wa chombo chake.

Mkurugenzi wa TIRA, Zakaria Muyengi, alisema walibaini magari mengi hayana bima na mengine siyo halali hivyo ili kuthibiti walikubaliana kuwapo kwa mfumo wa kieletroniki wa kudhibiti vitendo vya kughushi bima na tayari umeanza kazi na kuwapo na kituo cha ukaguzi.

# Mikopo ya NMB kwa walimu yamkosha RC

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MKUU waq Mkoa wa Morogoro, Marthin Shigela, ameitaja Benki ya NMB kuwa ndio benki pekee nchini iliyotoa mikopo kwa watumishi wa serikali kuu na serikali za mitaa, huku walimu wakiwa wanufaika wakubwa zaidi.

Shigela alitoa kauli hiyo wakati wa kongamano la siku ya walimu lililoandaliwa na benki hiyo na kuwahusisha walimu wote wa mkoa huo pamoja na maofisa elimu.

Alisema serikali inatambua mchango wa NMB katika kuwathamini walimu na watumishi wa serikali kuu na serikali za mitaa kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu.

Alisema mikopo kwa watumishi imekuwa msaada katika kukidhi mahitaji mbalimbali katika ngazi ya familia hata kufanikisha maandalizi yao kwa maisha ya baadaye wanapostaafu.

"Natoa rai kwenu walimu kutumia fursa hii kwa kujifunza masuala ya kibenki ikiwamo mikopo, bima, na huduma mbalimbali za NMB ambazo zitawasaidia sio tu kupanua uwezo wenu kiuchumi bali pia kujenga utamaduni wa kuweka akiba ili kukithi mahitaji ya dharura pindi yanapojitokeza."alisema Shigela.


Naye Meneja mwandamizi mikopo kwa watumishi na taasisi za serikali NMB, Emmnuel Mahodanga, alisema benki hiyo imeona ni muhimu kukutana na wadau wake wakubwa katika huduma za kibenki kuzungumza nao na kuwapa maendeleo ya benki yao.

Mahodanga alisema kongomano hilo linalenga pia kuwapa uelewa zaidi wa huduma za benki hiyo ambapo wanaamini kupitia walimu zaidi ya 150 watasaidia kupeleka elimu kwa wenzao.

Mmoja wa walimu, Grace Njau , alisema kongamano hilo limekuwa na tija kwao kwani wametambua fursa na matumizi zaidi ya kidigital kutumia simu kwa kuunganishwa na huduma za NMB.

## Mwigulu anapotetea kodi na tozo umiza

Ukurasa 12




# siasa

JUMATANO JULAI 21, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe





Ukurasa 13

## Mwaka mmoja bila Mkapa anakumbukwa kwa haya

Na Sabato Kasika

# WARIOBA & KATIBA MPYA

## Wanasiasa wamuonyesha anapoteleza, kujichanganya



Mwenyekiti wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashim Rungwe



Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya.

WIKI moja baada ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Jaji Joseph Warioba, kupigilia msumari kuhusu umuhimu wa taifa kupata katiba mpya, baadhi ya wadau wamekubaliana naye lakini wengine wamkosoa kwa kusema kuwa 'anaona wanaodai katiba ya wananchi akiwasikiliza inaelekea wanataka katiba ya kuwanufaisha kisiasa.

Aidha, wanashangaa kukubaliana na maelezo kuwa katiba mpya isubiri kwanza kuimarika uchumi, wakisema huko ni kujichanganya pia.

Kila mmoja kwa wakati wake, wanasiasa wanaozungumza na Nipashe, wanakubaliana na Jaji Warioba kuwa katiba ni ya muhimu, lakini kuna sehemu anateleza kidogo katika maelezo yake.

Wengine wanasema, katiba mpya ni muhimu, ila bado kuna haja ya kukubaliana na hoja ya Rais Samia Suluhu aimarishe uchumi, kwa kuwa mchakato wa kupata katiba unahitaji fedha.

Hayo yanajiri kutokana na kile ambacho Warioba, alikisema kwenye kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na ITV hivi karibuni.

Katika mahojiano hayo, Jaji Warioba anataka maoni ya wananchi yasipuuzwe, kwa kuwa ndiyo mara yao ya kwanza walishirikishwa kutengeneza katiba, huku akitahadharisha kuwa mtu asijekusema siyo muhimu wakati wananchi wanaeleza kuwa ni ya ulazima.

Hata hivyo, anashangaa kuwasikia wanaosema wanataka katiba ya wananchi, na kwamba wakati mwingine akiwasikiliza anaona kama wanataka katiba ya wanasiasa, kwa kuwa wanachozungumzia ni Tume Huru ya Uchaguzi, Rais kuchaguliwa kwa asilimia zaidi ya 50, na pia matokeo ya urais kupingwa mahakamani na kuwa na mgombea huru.

Kauli hiyo ndiyo ambayo inapingwa na wanasiasa wakidai kuwa, si kweli kwamba katiba hiyo inayotafutwa ni ya wanasiasa, bali kwa ajili ya Watanzania wote, kwa kuwa wanatamani uchaguzi huru.

### WARIOBA AMETELEZA

Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya, anasema, kilichosemwa na Jaji Warioba ni sahihi, lakini anatofautiana naye sehemu moja ambayo ni kuhusu kauli kwamba wanaodai katiba, wanataka katiba ya wanasiasa.

“Mimi ninakubaliana na kile alichosema Jaji Warioba kwa asilimia 100, lakini kudai kwamba wanasiasa wanaodai katiba mpya siyo ile wananchi ninadhani hapo ameteleza kidogo,” anasema Sakaya.

Anafafanua kuwa vyama vya upinzani vinataka tume huru ya uchaguzi, mamlaka ya Rais kupunguzwa, na pia matokeo ya uchaguzi ya urais yapingwe mahakamani, kwa kuwa ni miongoni mwa matakwa ya wananchi, na kwamba hilo si hitaji la wanasiasa tu.

Anasema, CUF ndiyo walioanza kudai mchakato wa katiba muda mrefu na kuongoza vyama vya upinzani kususia Bunge Maalum la Katiba, kutokana na kile walichodai kwenda kinyume maoni ya wananchi.

“Kama unakumbuka, Profesa Lipumba ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), kwa hiyo tunachohitaji ni katiba ya wananchi siyo ya wanasiasa kama alivyosema Jaji Warioba,” anasisitiza.

Anasema, pamoja na hayo, CUF inaunga mkono alichosema Jaji Warioba ingawa wanatofautiana kidogo, lakini anaamini ujumbe umefika, ambao ni kutaka kurejeshwa kwa mchakato wa Katiba Mpya.

“Pamoja na hayo, ninasisitiza msimamo wa chama chetu tulioutoa mwaka jana baada ya uchaguzi mkuu kwamba hatutashiriki uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 hadi kuwe na katiba mpya,” anasema.


### WAPE WANACHOTAKA

Mwenyekiti wa Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), Hashim Rungwe, anasema, kuzuia hitaji la Watanzania kwa

INAENDELEA UK. 12

# Mwigulu anapotetea kodi na tozo umiza

## Anataja tatizo ni kupenda vya bwerere




**Na Mwandishi Wetu**

BAJETI ya serikali iliyopitishwa na kuanza kutumika Julai 1, 2021 ambayo ni ya kwanza kwa awamu ya sita, imeanza na kupingwa kwenye tozo za miamala ya simu na bei ya mafuta.

Tozo hizo zimelalamikiwa kupindukia zikionekana kama zinawaumiza wananchi maskini licha ya kuwa zilibuniwa na kuwekwa kwa nia njema ya kutaka kuinua maisha hasa vijijini.

Katika mahojiano na ITV kwenye kipindi cha Dakika 45 juzi, Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba, anasema tozo za miamala ya simu ni kodi ya mshikamano inayotolewa na Watanzania wenyewe ili kujiletea maendeleo endelevu kwa mikono yao bila kutegemea misaada.

Akizungumzia miamala anasema walipa kodi wakubwa nchini ni 504, wakati waliosajiliwa kulipa kodi ni milioni 3.1 lakini wanaopokea huduma zote kuanzia maji, umeme, barabara, ulinzi ni milioni 60 kwa hiyo ni wakati wa kila mmoja kuwajibika kuchangia maendeleo ya taifa.

Nchemba anasema sekta isiyo rasmi isiyolipa kodi ni kubwa mno kuliko nchi jirani na kwamba watu wanapenda kuona mambo bwerere kama hiyo ili wasichangie maendeleo.

"Hata mwenye gari akinunua ndizi kwa mama anayeziuza kwenye beseni anamwambia punguza ni aibu. Tufanye mapinduzi na kuachana na kuona kuwa bwerere ni jambo la faida."

Anasema: "Ni lazima watu wachangie kupitia tozo ya muamala, waone fahari kulipia na kuchangia kodi kwa maendeleo yao. Iwapo watatumia Sh. 50,000 kuongea kwa simu kwa mwezi, haiwezekani kushindwa kuchangia fedha kidogo kwa ajili ya maendeleo."

Aeleza kushangazwa na watu wasiosikitika kuwa wanafunzi 11,000 wanashindwa kwenda vyuo vikuu kwa kukosa mikopo.

"Lakini pia hakuna maji shuleni watoto wanakwenda na galoni za maji shuleni ni aibu na taifa haliwezi kuendelea na utaratibu huo ndiyo maana hizo tozo tumeziweka" anasema Nchemba.

### NYONGEZA MAFUTA

Anasema Sh. 100 iliyoongezwa kwa lita ya mafuta imekuwa kilio kutokana na kupandisha gharama za maisha na Waziri Nchemba anawaambia wasikilizaji kuwa bajeti imeongeza Sh. 100 lakini pia wazalishaji mafuta duniani wamepandisha bei na sasa pipa ni Dola 72 (zaidi ya Sh 166,000).

Anasema licha ya ongezeko hilo tozo ya Sh. 100 imewekwa ili kuuongezea nguvu mfuko wa barabara uboreshe miundombinu hiyo vijijini.

Anasema takribani kilometa 100,008 ni mbovu na zinazidi kuharibika kila siku mvua zinaponyesha.

"Serikali imeongeza tozo kuwezesha kusafirisha bidhaa kutoka mazao yanapozalishwa na kuyafikisha sehemu zenye uhitaji, lakini si kufungua uchumi na uzalishaji vijijini pekee, bali pia kuokoa maisha." Anatetea tozo.

### MADHARA KIAFYA

Anasema kodi ya mafuta inaokoa maisha: "Kuna madhara kwa maisha ya binadamu kama hakuna barabara, kwa mfano, mvua za utangulizi zikinyesha zinazibomoa na akitokea mgonjwa au mjamzito mwenye uchungu ni lazima abebwe na machela tena wanaomsaidia wavue viatu. Ni hatari zaidi" anasema Waziri.

Anazidi kuitetea kuwa kutokana na hadhi na umri wa Tanzania hayo si mambo ya kuendekeza tena, na kuhoji wananchi wanaogopa nini kuongeza hiyo Sh. 100 iwapo kuna tija?

Anakumbusha kuwa bei ingepanda hata kama serikali isingeongeza tozo. OPEC ikapandisha bei zingepokelewa bila faida ya kimkakati hivyo hakuna sababu ya kuendelea kusikitika, anasisitiza.

Katika Sh. 100 inayoongezwa malengo ni kuokoa maisha ya wajawazito na wagonjwa lakini pia ni mkakati wa kufungua maendeleo kwa kukiwezesha kila kijiji.

"Mvua ikinyesha watoto wanashindwa kurudi nyumbani maji yamejaza mto wanalala kwa jirani. Watanzania wakumbuke kuwa ukisafirisha bidhaa kutoka sehemu yenye barabara mbovu bei yake ni kubwa zaidi kuliko ile yenye lami, hivyo barabara zisizopitika hupandisha gharama za maisha.

### MAFUTA NAFUU

Nchemba anapoulizwa inakuwaje mafuta nchini Zambia na Burundi ni nafuu licha ya kwamba yanapitia katika bandari ya Dar es Salaam?

Anajibu kuwa tofauti ni ukubwa wa uchumi, uchumi wa mataifa hayo ni mdogo ukilinganishwa na Tanzania na kwamba ni kanuni ya kiuchumi mahitaji yakiwa makubwa bei hupanda na yakishuka bei hupungua pia.

Anatetea kodi hizo kuwa, serikali imeongeza nguvu ili kuzikarabati barabara za vijijini kwa lengo la kuimarisha huduma za kijamii lakini pia kuwezesha wakazi wa vijijini kuwa na maisha bora.

### KWANINI MALALAMIKO?

Inawezekana kodi na tozo zikainua maisha na kuwezesha wengine kujiajiri na kupunguza, umaskini, utegemezi na kuhama kutoka mashambani kwenda mijini, lakini zinawaumiza wananchi, ziangaliwe kwa jicho jingine.

Masuala ya tozo za simu yanahitaji uhamasishaji, moyo wa kizalendo tena uzalendo wa hali ya juu kwani watu wengi wanaona kama kuna baadhi ya maeneo watu hawatozwi kodi na hayo serikali ianze kuyatoza.

Lakini matumizi mabaya ya fedha za umma yanawaumiza, Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwapo ufisadi, wizi na ubadhirifu kila mwaka, mambo yanawafanya walipakodi waone kuwa fedha zao zinaliwa.

Aidha, kunung'unikia kodi kunatokana na ukweli kuwa watumishi wa umma wanadaiwa kuwa matajiri kuliko wafanyabiashara ndiyo maana kuna hofu kuwa hela wanazolipa huenda zinaliwa na wachache huku maendeleo yao hasa vijijini yakidumaa.

Pengine ni wakati wa kuwauliza wananchi kwanini wanakataa au kulalamikia baadhi ya kodi? Pia kurekebisha na kukomesha ubadhirifu na kuwatoza kodi baadhi ya wale wasiolipa.

# WARIOBA & KATIBA MPYA

**INATOKA UK. 11**

sababu ya kutaka kuimarisha uchumi ni kutowatendea haki.

"Siamini kwamba mchakato wa katiba mpya unasababisha kukwama kwa uchumi, kwani hiyo ni kama shughuli nyingine za maendeleo zinazofanyika sehemu mbalimbali nchini," anasema Rungwe.

Anafafanua kuwa serikali inatenga fedha kwa shughuli za maendeleo, itenge pia kwa ajili ya mchakato wa kupatikana mpya ambayo anaamini inaweza kusaidia nchi kwenda mbele zaidi kimaendeleo.

"Ninasema hivyo, kwa sababu katiba yenye maoni ya Watanzania inakuwa na mambo mengi ya muhimu ambayo wanataka wafanyiwe kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla," anasema.

Rungwe pia anakumbusha kwamba, Watanzania waliambiwa uchumi wa nchi uko imara, lakini anashangaa kusikia serikali ya awamu ya sita kusema umevurugika inataka iuimarishe kwanza.

"Pamoja na hayo, ninamuomba Rais Samia aruhusu mikutano na hadhara ya vyama vya upinzani ambayo ilizuiwa kinyume cha taratibu, kwani si sahihi kuzuia wakati viongozi wa CCM wakiendelea na mikutano kama kawaida," anasema.

### TUANZE NA UCHUMI

Kada wa CCM, Thomas Ngawaiya anasema, katiba hiyo inahitajika, lakini anafafanua kuwa kuna haja ya kusubiri kwanza ili kujiweka sawa kiuchumi, kwa kuwa mchakato huo unahitaji fedha.

"Binafsi sipingani na mzee wa Warioba, lakini ni vyema kuzingatia kile ambacho Rais Samia alikisema kwamba anahitaji kuimarisha uchumi kwanza ndipo mchakato huo uendelee," anasema Ngawaya.

Kada huyo anasema, bila kuwapo kwa fedha mchakato hauwezi kufanikiwa, hivyo kwa kuwa katiba iliyopo inaendelea kutumika ingawa ikiwa na viraka, iendelee kufanya kazi wakati Rais akiendelea kujipanga.

"Lakini pia ukitafakari sana, utagundua kuwa alichosema Jaji Warioba kwamba wanasiasa wanang'ang'ania katiba ambayo ni kwa maslahi yao utakuta ni kweli licha ya madai yao kupitia mgongo wa wananchi," anasema.

Mwanachama hiyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzannia (CEGODETA), anasema ingawa kuna haja kuwapo katiba mpya, bado Watanzania wanaweza kuwa kama Wamarekani.

"Katiba ya Marekani ina zaidi ya miaka 300, lakini wanaitumia kama kawaida na maisha yanaendelea, hivyo hata sisi tunaweza kuendelea na hii iliyopo ikiwa na viraka vyake wakati tukijipanga kuimarisha uchumi kwanza," anasema.

Anasema, Rais ameomba apewe nafasi ya kushughulikia uchumi kwanza, na kwamba kauli hiyo ilitosha kuwafanya wanasiasa kuelewa umuhimu wa uchumi ili kupata fedha za kurejesha mchakato wa katiba mpya.



Mkapa katika harakati za kisiasa enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

# Mwaka mmoja bila Mkapa, anakumbukwa kwa haya

## Ana kivuli uuzwaji NBC, mabadiliko NEC

**Na Gaudensia Mngumi**

JULAI 24, mwaka 2020, haikuwa siku salama kwa Watanzania maana waliamshwa na taarifa za kifo cha kiongozi wao aliyewaongoza kwenye awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Mkapa au Ben ni kama alifariki ghafla, kwa vile habari za ugonjwa wake hazikufahamika na wengi, kama ilivyokuwa kwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

Ben ameondoka, lakini anasifika kwa kuanzisha taasisi imara za umma ikiwamo Mamlaka ya Mapato (TRA) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), MKURABITA na kufungua uchumi mambo ambayo hadi sasa yanafanyakazi na kunaendelea kuimarisha maisha ya Watanzania.

Ni kiongozi ambaye aliweka vizuri mambo yake kwa kutumia taaluma ya kidiplomasia aliyokuwa amebobea, na moja ya mambo aliyoyafanya ni kuungwa mkono na mashirika na taasisi za kimataifa likiwamo Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia (WB) na wadau wengine ambao walisaidia juhudi za kufufua na kuinua uchumi wa Tanzania.

Akiwa amezaliwa mwaka 1938 katika Kijiji cha Lupaso –Masasi mkoani Mtwara, ni zao la Uhuru wa Tanzania kwa vile alishuhudia bendera ya Muingireza ikishushwa na kupandishwa ya Tanganyika mwaka 1961 akiwa na miaka 23.

Ni miongoni mwa vijana waliozijua siasa za kupinga ukoloni, walithamini misimamo ya kimapinduzi kama uhuru na kazi, ubeberu na ukoloni ni unyama na hamu yake ilikuwa kama chama kilicholeta uhuru cha TANU, kuona Tanzania inaendelea na kujitegemea.

Ingawa alifariki miezi michache baada ya kuzindua kitabu chake cha My Life, Ma Purpose: A Tanzanian President Remembers, amewaachia Watanzania na dunia yale yote aliyopitia na namna ambavyo kwa asili ni mpenda maendeleo pamoja na mleta mabadiliko.

### NGUZO YA MAWASILIANO

Mkapa anasifika kwa kuwa kinara wa soko huria na kubadilisha muundo wa mashirika na sekta ya umma. Akianza kuipangua sekta ya mawasiliano na kuundoa ukiritimba wa Shirika la Posta na Simu (TPTC) na kubariki ujio wa wa kampuni za simu za mkononi za Tritel na Mobitel.

Kazi yake imeifanya Tanzania kuwa miongoni mwa mataifa duniani ambayo watu wake wengi wanatumia simu za mkononi kwa mawasiliano na kwenye uwekezaji.

Kwa mujibu wa hotuba ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano hadi Aprili mwaka huu, Watanzania wanaomiliki simu za mkononi ni milioni 53.

Kwa upande wa intanet wapo watumiaji milioni 48.9 hadi, wakati laini za simu zilizosajiliwa kwa vidole ni milioni 53, kwa mujibu wa takwimu za wizara hiyo, ilipowasilisha bajeti Juni mwaka huu.

### UJIO BENKI BINAFSI

Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizokuwa hazina benki za kutosha na huduma za fedha zilikuwa zinafuata mkondo wa kizamani, lakini awamu ya Mkapa ilisimamia uanzishwaji wa benki nyingi binafsi na maduka ya kubadilisha fedha (bureau).

Aidha, aliasisi uanzishwaji wa benki za wananchi (community) ikiwamo Dar es Salaam, Mwanga, Mufindi, Tandahimba na Mbinga (Community Banks)

Aidha, aliendeleza taasisi za kifedha (micro finance) zisizokuwa za kibenki ambazo ziliendelea kuhudumia mijini na vijijini hata kule kusikokuwa na huduma za benki.

### MKURABITA

Mkapa anaweza kuitwa baba wa kuondoa umaskini kwa imani kuwa mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe .

Ndiye mwanzilishi wa Mkakati wa Kurasimisha Mali za Wanyonge (MKURABITA) uliokuwa unalenga kurasimisha makazi, biashara, ardhi na mali zote zikiwamo zilizojengwa kwenye makazi duni na ardhi ambayo haijapimwa.

MKURABITA ulilenga mali hizo kupata vibali na uhalali wa kisheria ili zitumike kuondoa umaskini kupitia mikopo na alikuwa akireja mali hizo kama "dead assets" au 'mitaji mfu.'

### BABA WA ELIMU

Mkapa hakuisahau sekta ya elimu, alianza na mkakati wa kuendeleza elimu ya msingi (MMEM), sekondari MMES, akaanzisha mpango wa elimu ya msingi kwa walioukosa MEMKWA, zote hizo zilikuwa ni jitahada za kuwaamsha Watanzania kutoka kwenye lindi la umaskini ambao pia ulichangiwa na kukosekana elimu bora. MMES na MMEM ulijenga sekondari na madarasa, nyumba za walimu, katika maeneo mengi nchini.

Ulifanikisha kuchonga madawati, kufunza walimu na kuanzia hapo juhudi za kuboresha elimu ya awali, msingi na sekondari zimekuwa na suala endelevu, zama hizi serikali ikiondoa ada na kugharamia elimu ya awali hadi sekondari.

### UJIO SHULE BINAFSI.

Katika awamu yake aliruhusu taasisi za dini, jumuiya mbalimbali na sekta binafsi kuanzisha shule za awali, msingi, sekondari, taasisi za elimu ya juu na serikali kuziunga mkono kwa kila hatua.

Kwa mujibu Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) Tanzania ina vyuo vikuu vya umma 12 na vya binafsi 32, hatua iliyoanza na awamu ya Mkapa.

### MTANGAMANO

Wakati wa awamu yake, Mkapa alikuwa kinara wa kusimamia uundwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kazi iliyoanzishwa na mtangulizi wake Rais Ali Hassan Mwinyi.

Pia alishiriki bega kwa bega kuiboresha zaidi Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na kuipa majukumu makubwa kiuchumi baada ya harakati za ukombozi.

Aidha, alikuwa kinara wa kuundwa kwa Umoja wa Fordha wa Nchi za Kusini mwa Afrika (COMESA) na aliendelea kusimamia uwepo wa umoja huo.

### ANAPOKOSOLEWA

Katika uongozi wake wa miaka 10 kuanzia 1995 hadi 2005, Mkapa amefanya mengi. Lakini hataacha kukosolewa. Wengine wangetegemea kuona akisimamia mabadiliko ya katiba na kuwezesha kupata katiba mpya inayoakisi uwepo wa vyama vingi.

Aidha, kuunda Tume Huru ya Uchaguzi (NEC) na kubadilisha sheria za uchaguzi kwa kuwa ndiye aliyekuwa baba wa mageuzi na msimamizi wa siasa za vyama vingi kwenye uchaguzi wa 1995.

Mwaka 1995 alikuwa mgombea urais wa kwanza wa CCM kwenye uchaguzi ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa na ndiye aliyekuwa kiongozi wa kuanza kuzitekeleza siasa za mabadiliko ya mifumo ya siasa za vyama nchini, kwa vile Tanzania ilikuwa taifa la chama kimoja kwa miongo mitano.

Mkapa ilitegemewa, ili kudumisha demokrasia, angeiunda upya NEC na sheria za uchaguzi ili uwanja wa demokrasia usiwe na mabonde na milima kama ilivyo sasa, kwani kutoangaliwa eneo hilo kumekuwa ni changamoto ya kisiasa inayoitafuna Tanzania hata leo. Kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi 1995 hadi wa mwaka jana 2020, kilio cha wanasiasa, wapinzani na wanaharakati wa demokarasia na uliberali kimebakia kuwa NEC na sheria za uchaguzi ni kikwazo cha kuwapo uchaguzi huru na haki nchini.

### UBINAFSISHAJI ULIVYOKUWA

Mkapa alifungua milango na njia za uchumi na kualika wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi. Aliboresha na kubadilisha muundo wa mashirika ya umma kupitia ubinafsishaji.

Kwenye eneo hilo, mashirika na kampuni za umma ziliuzwa kwa wawekezaji wa kigeni wengi kutoka Afrika Kusini.

Mkapa anakosolewa kwenye ubinafsishaji wa benki ya NBC, Shirika la Ndege, la Reli, miradi ya kuboresha TANESCO kupitia Net Group Solution ya Afrika Kusini na kubinafsisha kitengo cha makontena cha bandari ya Dar es Salaam.

Katika kitabu chake anakiri na kuomba radhi kuwa, kwenye ubinafsishaji 'alichemka'. Lakini anawasihi Watanzania kumsamehe kutokana na ukweli kuwa wakati wa uongozi wake, yalitokea mauaji kisiwani Pemba mwaka 2001 na tafrani nyingine nyingi zilizoibuka baada ya uchaguzi wa mwaka 2000.

Anasema hilo lilimuumiza, lakini angependa watu kusamehe na kusahau kwa kuwa, ni wakati wa kuangalia yaliyofanyika Pemba yasijirudie tena kwingine.

JUKWAA LA VIONGOZI

# NELSON MANDELA

## ▮Mtu wa kipekee anayezidi kutukuka
## ▮UN yamuenzi kuadhimisha 'MandelaDay'



Nelson Mandela siku yake inaadhimishwa kila mwaka Julai 18. **PICHA MTANDAO.**

**Na Christina Mwakangale**

DESEMBA 5, 2013 ni siku aliyofariki dunia Nelson Mandela, Rais wa kwanza mweusi wa Afrika ya Kusini.

Ni kiongozi wa kipekee na wa aina yake, hivyo Umoja wa Mataifa (UN) unapomtafakari shujaa huyo, unaitangaza Julai 18, kila mwaka kuwa Siku ya Mandela.

Siku ya Kimataifa ya Mandela imeanzishwa na UN ili kumkumbuka, kumuenzi na kuutafakari kazi zake, utu wake, usawa aliusimamia na mpigania haki za binadamu namba moja.

Julai 18, 1918 ndiyo siku aliyozaliwa Mandela na imepitishwa rasmi na UN mwaka 2009 na maadhimisho ya kwanza yakafanyika mwaka 2010.

Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres, katika ujumbe wake kwa siku hiyo mwaka 2010, anasisitiza dunia kumkumbuka na kumuenzi Mandela kwa kutafakari utu wake, usawa pamoja na haki za binadamu alizozitetea na kuzisimamia.

Anamsifu kuwa alikuwa mstari wa mbele, kupinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini na kwamba kila binadamu akitumia uwezo wake anaweza kuifanya dunia mahala bora pa kuishi kama kiongozi huyo alivyofanya.

"Kila mtu ana uwezo na jukumu la kuibadili dunia kuwa bora zaidi. Siku ya Mandela ni fursa kwa kila mtu kuchukua hatua na kuhimiza mabadiliko. Kila mwaka, katika siku hii ya kuzaliwa ya Nelson Mandela, tunamshukuru mtu huyu wa ajabu aliyejumuisha matakwa ya juu zaidi ya UN na dunia."

"Tumeshuhudia sasa jamii zikizidi kuparaganyika, lugha za matusi na uongo zimeongezeka, habari zinazofifisha ukweli, kuhoji sayansi na kudhoofisha taasisi za kidemokrasia," anasema Gutteres.

Anasema janga linaloendelea la COVID-19 linachangia kurudisha nyuma maendeleo na vita dhidi ya umasikini, pia katika kipindi cha matatizo waliopo kwenye makundi yenye kuhitaji msaada, wanaoteseka zaidi, na kulaumiwa ingawa hawana hatia kwa yaliyotokea.

"Janga hilo la corona limeonyesha umuhimu wa mshikamano na umoja, maadili yaliyopigiwa chepuo na Nelson Mandela katika kipindi cha uhai wake kwa kupigania haki na usawa."

"Hakuna aliyesalama mpaka wote tuwe na usalama. Na kila mmoja wetu ana jukumu la kufanya." anasema Guterres katika ujumbe wake wa siku ya Mandela, mwaka huu.

Katibu Mkuu wa UN, anasema watu wote wanatakiwa kuhamasika na ujumbe wa 'Madiba' kwamba kila mmoja anaweza kuleta mabadiliko katika kutangaza amani, haki za binadamu, maelewano na utu kwa watu wote.

> "Hakuna atakayetulia duniani, iwapo umaskini, ukosefu wa haki na usawa vitaendelea kushamiri," anasema Mandela katika moja ya nukuu zake.

"Katika kuyaenzi maisha ya Madiba, tuheshimu wito wake na kuchukua hatua na kutiwa nguvu na urithi aliotuachia."

### MANDELA NI NANI

Nelson Mandela ndiye Rais wa kwanza mweusi Afrika Kusini, baada ya kutumikia kifungo cha miaka 27 gerezani katika kisiwa cha Robben.

Pamoja na wapigania uhuru wengine, aliachiwa huru mwaka 1990 baada ya kusota kwa miongo mitatu.

Mandela au Madiba alihimiza mshikamano na kukomesha ubaguzi wa rangi, jambo ambalo sasa lipo hatarini kwani mshikamano wa kijamii duniani unatishiwa na mgawanyiko.

Wakati Nelson Mandela alipokuwa kijana, Wazungu na Waafrika walikuwa hawaishi pamoja chini ya mfumo wa ubaguzi wa rangi uliojulikana kama 'apartheid'.

Weupe, ambao walikuwa idadi ndogo ya raia, ndiyo walioidhibiti nchi na njia zote za uchumi.

Ilikuwa ni marufuku kwa weusi kwenda shuleni, hospitali na hata maeneo ya kubarizi kama katika fukwe za bahari sawa na watu weupe.

Hali ilikuwa imeimarika zaidi katika shule na hospitali za watu weupe, wakati Waafrika walinyimwa haki msingi, kama kushiriki katika uchaguzi mkuu, lakini Nelson Mandela aliamini kwamba kila mtu anastahili kuchukuliwa kwa usawa.

Mandela alijiunga na Chama cha African National Congress (ANC) na baadaye kuongoza tawi la vijana la chama hicho, akishiriki maandamano kupinga utawala wa ubaguzi wa rangi.

### DUNIA ILIMTOA GEREZANI

Wakati Mandela akiwa gerezani, picha zake zilipigwa marufuku na ilikuwa ni kinyume cha sheria kumnukuu hadharani.

Hata hivyo dunia ilisimama kwa umoja na kufanya kampeni za kutaka aachiliwe, nyimbo ziliimbwa na matamasha makubwa yaliandaliwa kulalamikia kufungwa kwake.

Hatimaye mwaka 1990, Rais wa Afrika Kusini FW de Klerk, aliamuachia huru na alipotoka gezani na alipokelewa kama shujaa baada ya kuachiwa huru.

### KUSIMAMIA MSAMAHA

Mandela ana sifa na umaarufu wa kuhimiza msamaha, kuvumiliana na usawa baina ya watu.

Utawala wa ubaguzi wa rangi ulifutiliwa mbali mwaka 1991, na miaka mitatu baadaye, Afrika Kusini iliandaa uchaguzi wa kwanza mkuu ambapo watu weusi waliruhusiwa kupiga kura kama weupe.

### KUWA RAIS MAARUFU

Nelson Mandela alichaguliwa kuwa Rais mwaka 1994 na akaanza kuleta umoja baina ya watu wa rangi tofauti. Ilipotimia mwaka 1993, alipewa tuzo ya amani ya Nobel- ya kiwango cha juu na ya aina yake.

Hii ni kutambua jitihada zake na mwaka 1995, wakati Afrika Kusini ilipoandaa mashindano ya kwanza ya kombe la dunia la mchezo wa raga (rugby).

Mandela aliiunga mkono timu ya Afrika Kusini, iliyojumuisha zaidi Wazungu, jambo lililosaidia kuiunganisha nchi hiyo zaidi na kusahau yaliyopita.

Mandela ni mmojawapo ya viongozi maarufu duniani, huku wanasiasa na nyota wa aina mbalimbali walikuwa wakipanga msururu ili kupigwa picha pamoja naye.

"Hakuna atakayetulia duniani, iwapo umaskini, ukosefu wa haki na usawa vitaendelea kushamiri," anasema," anasema Mandela katika moja ya nukuu zake.

### MAMBO YAKE HADI KIFO

Baadhi ya vitabu alivyoandika Mandela ambavyo vinasomwa karibu duniani kote ni pamoja na "I Am Prepared to Die", Long Walk to Freedom, Mandela: The Authorised Biography, Conversations With Myself, Dare Not Linger na The Presidential Years.

Mandela aliwahi kuonekana katika filamu mbalimbali ikiwamo, Death of Apartheid Mandela: Son of Africa, Father of a Nation, Mandela and de Klerk, Goodbye Bafana, Endgame, Invictus na Winnie Mandela.

Alifariki dunia Desemba, 5 mwaka 2013 akiwa na miaka 95. Angekuwa bado hai leo angefikisha miaka 103.

***Kwa msaada wa vyanzo mbalimbali***



## DC aona shida wadau EWURA

Na Augusta Njoji, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Kondoa amesema kukosekana kwa elimu kwa jamii kuhusu udhibiti unaofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kumekuwa chanzo cha kuibuka kwa malalamiko.

Khamis Manachi, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alitoa kauli hiyo jana alipofungua semina kwa Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAWAVITA), iliyoandaliwa na EWURA.

Alisema taasisi nyingi na hata mtu mmoja, linapokuja suala la udhibiti, huona kama wanaonewa kutokana na kukosekana kwa uelewa kuhusu shughuli za mdhibiti.

"Nimearifiwa kuwa kutokana na majukumu ya EWURA kugusa Watanzania wengi na ili kuondoa pengo la uelewa wa huduma zake, ndiyo maana EWURA imekubali ombi la TAWAVITA la kufundishwa kuhusu shughuli za EWURA," alisema.

Alisema ni vyema kuhakikisha watumiaji wa huduma za EWURA wanajua wajibu na haki zao.

"Ninafahamu kuwa ninyi ni sehemu muhimu yawatumiaji wa huduma za EWURA, inawezekana kuna mafundi umeme humu ndani ambao inabidi wawe na leseni za EWURA, inawezekana kuna wamiliki wa vituo vya mafuta ambao inabidi wawe na leseni za EWURA au tunaweza kuwa na wamiliki wa kampuni za kuzalisha na kusambaza umeme huko tulikotoka inabidi ziwe na leseni za umeme," alisema.

Kiongozi huyo alisema anaamini semina hiyo itasaidia azma ya serikali ya kuwasaidia Watanzania kutambua haki na wajibu wao kwa jamii.

Aliipongeza EWURA kwa kutoa semina hiyo ambayo anaamini itasaidia watu wenye ulemavu wa kusikia kuwa na uelewa wa shughuli za EWURA.

Akiwasilisha mada, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, aliwataka washiriki kuhakikisha wanachukua risiti kila wanapopatiwa huduma za maji na nishati ili iwe rahisi kusaidiwa na EWURA pindi inapotokea tatizo.

Pia, aliwataka washiriki 30 ambao ni mafundi wa umeme kuhakikisha wanakuwa na leseni kutoka EWURA ili kuwafanya kazi zao vizuri.

"Kwa sasa hakikisha hamruhusu fundi kuwatandazia nyaya kwenye nyumba zenu kama hana leseni za EWURA, hivyo ninyi mliopo humu na mhamasishe wenzenu kuwa na leseni ili muweze kufanya kazi zenu kwa ufanisi na uhuru," alisema.

Katibu Mtendaji wa Taasisi hiyo, Kelvin Nyema, alisema chama chao kimefikia hatua ya kuomba kupatiwa mafunzo hayo ili wajengewe uwezo mafundi umeme na mafundi wa nyumba ambao ni viziwi.

"Miongoni mwa viziwi, wapo mafundi wa umeme, mafundi ujenzi wa nyumba na tunajua tunahitaji leseni lakini hatujui nini cha kufanyeje, pia viziwi ni watumiaji wa maji na nishati na ndiyo maana tunahitaji mafunzo," alisema.

# Walimu 120,000 wapandishwa vyeo

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ametaja mafanikio yaliyopatikana ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo walimu waliotimiza vigezo 119,887, wapandishwa madaraja.

Akizungumzia mafanikio hayo jana jijini hapa, waziri huyo alisema walimu hao ni kati ya 122,574 waliokasimiwa, sawa na asilimia 97.8. Pia, alisema kwa kipindi hicho walimu 622 walisajiliwa na kupatiwa namba ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Pamoja na hayo, alisema serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ambapo Sh. bilioni 152.1 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa ya shule za msingi na sekondari huku kiasi cha Sh. bilioni 17.5 kikitolewa na kupokewa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya maabara 582 za sayansi katika halmashauri mbalimbali nchini.

"Kiasi cha Sh. bilioni 8.8 kimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 110 kwa baadhi ya shule za sekondari zenye shida ya wanafunzi kutembea umbali mrefu.

"Hiyo imeendelea kuongeza wigo wa wanafunzi waliofaulu kutoka kidato cha nne kwenda kidato cha tano ambapo katika kipindi hiki Wanafunzi 87,663 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano sawa na ongezeko la wanafunzi 14,562 kulinganishwa na wanafunzi 73,101 waliochaguliwa mwaka 2020,"alisema.

Ummy alisema kuwa katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, wanafunzi wote wasichana waliokidhi vigezo, wamechaguliwa kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya kati.

Kuhusu kutekeleza azma ya kuwapatia wanafunzi elimumsingi bila ada, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 83.2 ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia huku ikiajiri walimu 6,946 wa shule za msingi na sekondari na kufanya msawazo wa walimu kwenye halmashauri zote 184.

Akizungumzia eneo hilo, alisema kwa kipindi cha siku 100, serikali imepeleka kwenye halmashauri 34 kiasi cha Sh. bilioni 20.3 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri 34.

Alisema ujenzi wa hospitali hizo unaendelea na halmashauri 76 zimepelekewa fedha kiasi cha Sh. bilioni 11 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tatu kila halmashauri.

Vilevile, alisema kupitia mradi wa matokeo ya ufanisi (Result Based Financing -RBF), umefanyika uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya ambapo zahanati 279, vituo vya afya 46 na hospitali 22 za wilaya zimepatiwa fedha kiasi cha Sh. bilioni 30.8 ili kuviwezesha vituo hivyo kufika ngazi ya nyota tatu katika ubora wa utoaji huduma.

Kuhusu ukusanyaji mapato, Ummy alisema zaidi ya Sh. bilioni 178.9 zimekusanywa katika kipindi hicho na kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 15.6 zimetolewa kama mikopo kwa vikundi 3,757 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.



Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Asasi za Kiraia Tanzania Bara, Neema Lugangira (kulia), akikabidhi sehemu ya barakoa zenye thamani ya zaidi ya Sh. 2,000,000 kwa Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dodoma (CPC), Musa Yusufu, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya wanachama kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kanisa latia mkono ujenzi mradi elimu

Na Peter Mkwavila, DODOMA

KANISA la Pentecostal Church of Tanzania (FPCT) kupitia mradi wa elimu jumuishi unaotekelezwa Wilaya ya Bahi na Dodoma, limeahidi kuisaidia serikali kuhakikisha wanafunzi wenye uhitaji maalum shuleni wanapata misaada mbalimbali ya kielimu ili kufikia malengo yao.

Meneja mradi huo, Ibrahim Suleiman, aliyasema hayo juzi alipotoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Elimu Maalum, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Migeha Julius, kwenye hafla ya kutunuku vyeti kwa walimu waliohitimu mafunzo ya elimu maalum yaliyofanyika mkoani Dodoma.

Suleiman alisema mradi huo utahakikisha unaunga mkono jitihada za serikali katika kuwakomboa wanafunzi wenye uhitaji maalum.

Alisema kuwa mradi wa elimu jumuishi umekuwa ukihakikisha watoto wenye ulemavu wanapatiwa fursa bora ya kielimu na kufikia malengo yao.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Migeha Julius, alisema serikali imejipanga kuhakikisha upatikanaji wa misaada kwa wanafunzi wenye uhitaji maalum unakuwapo ili wafanye vizuri kitaaluma.

Julius alisema serikali imejipanga kuhakikisha misaada mbalimbali inatolewa kulingana na aina ya ulemavu itakayowasaidia kitaaluma ili wafanye vizuri katika masomo.

Aliwataka walimu waliohitimu mafunzo hayo ya elimu jumuishi kueneza ujuzi walioupata ili kupunguza mtizamo hasi kwa jamii.





# Chunya yaagiza tahadhari ya corona

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WILAYA ya Chunya imeagiza viongozi wa ngazi mbalimbali kujiridhisha kwanza na maandalizi ya kujikinga na maambukizi ya corona kabla ya kuruhusu sherehe ama kongamano lolote kufanyika.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon Mayeka, alitoa agizo hilo juzi alipokuwa anazungumza na wanachama wa vyama viwili vya msingi vya wakulima wa tumbaku vya Mtanila na Bitimanyanga AMCOS kwenye mkutano uliofanyika katika Kata ya Lupatingatinga.

Mkutano huo uliandaliwa maalumu kwa ajili ya kusaini mkataba wa mkopo wa bima ya afya kwa wakulima baina ya Benki ya Azania, Mfuko wa Bima ya Taifa (NHIF) na Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Chunya (CHUTCU).

Mayeka alisema kwa sasa katika Wilaya hiyo hakuna mtu aliyebainika kuugua ugonjwa huo, lakini kutokana na mwingiliano wa watu unaotokana na shughuli za kiuchumi, ni lazima hatua ziendelee kuchukuliwa za kujikinga.

Aliwaagiza viongozi wa Serikali kuweka maji tiririka kwenye ofisi zao ili mtu anayeenda kupata huduma anawe mikono kabla ya kuanza kuhudumiwa, huku akiwataka wananchi wote kuvaa barakoa kabla ya kuingia kwenye maeneo ya umma.

"Sherehe yoyote ambayo itaandaliwa ndani ya wilaya hii zikiwamo harusi na makongamano, tutatakiwa kujiridhisha kwanza na maandalizi ya kujikinga na corona, tukibaini maandalizi ni hafifu tutazuia, huu ugonjwa ni hatari sana na umekuwa ukibadilika badilika," alisema Mayeka.

Aidha Mayeka alisema hivi karibuni rafiki yake ambaye waliingia wote jeshini alifariki kwa ugonjwa huo wa Corona na kwamba muda mfupi kabla hajafariki waliwasiliana kwa njia ya simu na akamweleza kwamba alikuwa anaumwa.

Alisema wakati anampigia simu alibaini kuwa sauti yake ilikuwa ya chini na ilikuwa haisikiki vizuri na alipomuuliza kwanini hali ilikuwa vile, alimjibu kuwa anaumwa na alikuwa amelazwa.

"Siku moja baadaye alifariki kwa corona, sasa nikiangalia hata kwenye huu mkutano naona wengi wetu hapa hamjavaa barakoa, kitu ambacho ni hatari... sasa nawatahadharisheni tujikinge na ugonjwa huu, ukivaa barakoa unajikinga usipate maambukizi," alisema Mayeka. Akizungumzia mkopo wa bima, Meneja Mwandamizi wa Benki ya Azania, Jackson Lohay, alisema mkopo huo ambao wamewakopesha wakulima hauna riba na wakulima watalipa wakati wa mavuno ya tumbaku.

Alisema wanakusudia kuwanufaisha wakulima 700 wa kata za Bitimanyanga na Mtanila, na kwamba pamoja na familia zao wanufaika watakuwa zaidi ya 2,000 katika Wilaya ya Chunya pekee.

"Tunashirikiana na NHIF kwenye mpango huu kwa sababu sisi ni washirika wa muda mrefu, NHIF inamiliki hisa asilimia 17 ndani ya Azania Benki na kabla ya kuja huku tulianzia Kahama mkoani Shinyanga na Kagongwa mkoani Kigoma.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Meneja wa shirika hilo Mkoa wa Mbeya, Mbala Shitindi, alisema Wilaya ya Chunya ni miongoni mwa maeneo ya mkoa huo yenye wanachama wengi wa mfuko huo.

Alisema mwaka 2019 wanachama 2,500 kutoka wilayani Chunya walijiunga na mfuko huo lakini mwaka 2020 idadi ilishuka kutokana na atha ya corona kwenye kilimo pamoja na mmoja wa wanunuzi wa tumbaku kujitoa.



Wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Itumbi, wilayani Chunya, mkoani Mbeya, wakisaga mawe yenye madini hayo kabla ya kuanza uchenjuaji juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Jengo la mama na mtoto kujengwa kwa bil. 9/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHILINGI bilioni 9.2 zimetolewa na Serikali kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa jengo la mama na mtoto lenye urefu wa ghorofa sita katika Hospitali ya Wazazi (META) jijini Mbeya.

Hadi sasa jengo hilo limekamilika kwa asilimia 85, na kwamba linatarajiwa kutoa huduma ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu.

Akizungumza juzi baada ya kufanya ziara ya kukagua jengo hilo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alieleza kufurahishwa kuona maendeleo ya ujenzi huo na kwamba hadi litakapokamilika, litasaidia kuimarisha huduma ya afya ya mama na mtoto.

"Serikali yetu sikivu imetupatia fedha kiasi cha Sh. bilioni 9.2 ili wananchi wapate huduma bora za afya na kupunguza kero zinazojitokeza dhidi ya kinamama na watoto, mradi huu utakapokamilika idadi ya vitanda itaongezeka kutoka 150 hadi 400 lina vyumba vya kutosha na vitanda vya kujifungulia vya kutosha pamoja na vyumba vya upasuaji," alisema Dk. Gwajima.

Aidha, Waziri Gwajima alikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa wodi kwa ajili ya watu wanaohitaji kufanyiwa upasuaji linalojengwa pamoja na vyumba sita vya upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema jengo hilo litakuwa na vitanda 82 vitakavyolaza watu waliofanyiwa upasuaji au wanaosubiri kufanyiwa upasuaji na kwamba limegharimu bilioni tatu na kwamba makadirio ya Ujenzi wa jengo hilo ni Sh. bilioni 5.5

Alisema jengo hilo litapunguza mrundikano wa wagonjwa katika MZRH kwa ufadhili wa Shirika la Global Fund.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Chuwa Chuwa alimhakikishia Waziri Gwajima kwamba watasimamia maelekezo aliyoyatoa.

Alisema jumla ya Sh. bilioni 14 zimetolewa na Serikali kuboresha sekta ya afya mkoani Mbeya na kwamba wanaendelea kusimamia miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati.

## Homera ashauri wanaume wenye ndoa kutetewa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amekishauri Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kuanzisha utaratibu wa kusikiliza matatizo yanayowakabili wanaume kwenye ndoa, ukiwamo unyanyasaji ili wawasaidie.

Homera alitoa ushauri huo juzi alipokuwa anazindua jengo la TAWLA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini lililopo eneo la Sae jijini Mbeya ambalo litahudumia wananchi wa mikoa yote ya ukanda huo hasa wanawake na watoto.

Alisema pamoja na kwamba lengo la TAWLA ni kuyahudumia makundi ya wanawake na watoto kwenye eneo la kisheria, lakini pia wana wajibu wa kuwasaidia wanaume kwenye eneo hilo kwa maelezo kuwa nao wananyanyasika.

Alisema baadhi yao wananyimwa unyumba na wenza wao, lakini hawana sehemu ya kusemea hivyo kuanzisha utaratibu wa kuwasikiliza kutasaidia kuwaondolea mzigo wa msongo wa mawazo na matatizo ya kisaikolojia.

Alishauri utaratibu huo uende sambamba na kuwasikiliza wazee ambao wametelekezwa na vijana wao kwa kutoa ushauri na kama suala linahusu jinai walisimamie iasavyo kwenye ngazi za kisheria.

"TAWLA msijikite tu kwa wanawake, pia baadhi ya wanaume wanakumbana na changamoto ndani ya ndoa mfano kuna mtu alikuja ofisini kwangu kulalamika kuwa ananyimwa unyumba na mke wake ambaye ni muuguzi, masuala kama haya niwaombe muwe mnayashughulikia," alisema Homera.

Katika hatua nyingine mkuu huyo wa mkoa alimuagiza mkuu wa wilaya ya Mbeya ndani ya wiki mbili awe ametoa eneo kwa ajili ya kujenga ofisi kubwa ya chama hicho kanda.

Kwa upande wake mwenyekiti wa TAWLA, Lulu Ng'wanakilala, alisema chama hicho kina wanachama zaidi ya 300 nchi nzima wakiwamo wabunge, mawaziri, majaji, mahakimu, washauri wa kisheria na wanataaluma wa taaluma zingine.

Alisema uwapo wa ofisi hiyo mpya utaiwezesha TAWLA kufanya majukumu yake kiufanisi ya kutoa elimu ya kisheria kwa wanawake na watoto pamoja na kushughulikia changamoto za makundi hayo mahakamani.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama kuu Kanda ya Mbeya, Rose Ebrahim, alisema mahakama ipo tayari kushirikiana na chama hicho katika kusikiliza na kuamua haraka mashauri yanayohusu wanawake.



## SMZ yageukia utafiti, ubunifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis Juma, amesema serikali na taasisi za sayansi na utafiti zinachukua hatua za kuimarisha sera, utawala pamoja na taasisi katika kufanya utafiti na kuongeza ubunifu ili kuleta maendeleo endelevu.

Amesema hatua hiyo inafanyika kwa kutekeleza mradi wa kuimarisha mifumo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kufikia maendeleo endelevu kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Wizra ya Elimu, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ya Serikali ya Muungano na Tume ya Taifa ya UNESCO.

Katibu Mkuu aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mradi wa kuimarisha mifumo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kufikia malengo ya maendeleo endelevu, uliofanyika katika ukumbi wa Madinat Al Bahr, Mbweni mjini Unguja.

Alisema utekelezaji wa mradi huo umelenga na unahusisha maeneo makuu matano yakiwamo tathmini ya awali ya uwekaji wa alama ya mifumo ya kitaifa ya kisayansi, teknolojia na ubunifu; ushawishi wa kuyafanyia kazi mapendekezo ya sayansi na watafiti wa sayansi ya mwaka 2017.

Maeneo mingine ni ujenzi wa uwezo wa serikali, taasisi, watunga sera na wadau kubuni sera ya utekelezaji wa mradi huo. Pia kufuatilia utekelezaji wa mradi pamoja na maendeleo na utekelezaji wa mpango kazi wa vipaumbele vya kitaifa dhidi ya mradi huo.

Alisema amefarajika kuona ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na UNESCO Tanzania kwa kuandaa mkutano huo muhimu kwa lengo la kuwaleta pamoja wadau wa sekta ya umma na binafsi katika ngazi ya taifa ili kuchangia taarifa ya uandishi wa ripoti hiyo.

Pia alisema ana matumaini makubwa kuwa maazimio yatakayofikiwa yatachangia kwa kiasi kikubwa namna gani ya kushirikiana katika kuchangia uimarishaji wa mifumo ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika kufanya uamuzi shirikishi kwa lengo la kuimarisha maisha ya jamii na kujikinga na maradhi na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu katika nchi.

Aidha, alisema wizara yake iko tayari kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha wanatimiza azma ya mradi huo kwa maendeleo endelevu ya taifa.

Pia amewaomba wadau wote kuunga Mkono jitihada za Serikali na UNESCO pamoja na Taasisi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha uimarishaji wa mifumo ya Sayansi,Teknolojia na ubunifu, inapata nafasi ya kuchangia maendeleo ya kijamii na uchumi pamoja na kukinga jamii na majanga yanayotokana na matokeo ya tafifi za kisayansi.

# Mwinyi mgeni rasmi baraza la Eid

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, leo anatarajiwa kuongoza waumini wa dini ya kiislamu katika swala ya Eid-el hajj itakayoswaliwa katika viwanja vya Mnazimmoja Wete kisiwani Pemba.

Katika swala hiyo, Rais mwinyi pia alilihutubia Baraza la Eid katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete. Akizungumza na waandishi wa habari kisiwani Pemba, Mwenyekiti wa Kamati ya Sala na Baraza la Eid Kitaifa, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema Dk. Mwinyi anatarajiwa kuwaongoza wananchi wa dini ya Kiislamu katika sala hiyo.

Sheikh Khalid alisema hiyo ni fursa adhimu kwa wananchi kuswali pamoja na kiongozi wa nchi, hivyo ni vyema wakashiriki na kuhudhuria kwa wingi kwenye swala hiyo.

"Kwa kweli ni faida kubwa kwa kuja Rais kwani ni nafasi adhimu ya kiongozi huyo kujumuika pamoja na wananchi katika swala ya Eid, tujitokeze kwa wingi," alisema. Pia mwenyekiti huyo ambae pia ni Katibu wa Mufti Zanzibar, alisema Rais wa Zanzibar atalihutubia Baraza la Eid katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuwataka wananchi wote kufuatilia vyombo vya habari kusikiliza hotuba ya Dk, Mwinyi.

Alisisitiza kuwa ni muhimu kuisikiliza hotuba ya Rais kwa kuwa ni mwongozo, nasaha, dira na maelekezo ambayo ni muhimu kwa wananchi wa Zanzibar.

"Kwenye Baraza la Eid ni kwa watu maalumu si wananchi wote, hivyo tunawaomba wananchi wafuatilie kwenye vyombo vya habari ili wapate nasaha na mwongozo ambao utasaidia sana katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu", alisema.

Hata hivyo aliwataka kwa kila mwislam mwenye uwezo kuchinja siku hiyo kufanya hivyo kwa kuwa Eid el- Hajj ni sikukuu ya kuchinja na ni wajibu kwa kila mwislamu mwenye uwezo.

"Baada ya swala ya Eid mpaka siku ya tatu mbele unaweza kuchinja, hivyo tujitahidini kwa kila mwenye uwezo achinje kwani ni wajibu kwake na atapata fadhila kwa Mola wake," alifahamisha. Mwenyekiti huyo alisema siku 10 za mwanzo wa mwezi wa mfunguo tatu ni bora na kila amali inayofanywa na malipo yake ni makubwa kwa Mungu kuliko yanapoyafanywa siku nyingine, hivyo Waislamu wakithirishe ibada, kuomba dua, toba na kutoa sadaka kwa wingi.

Aliwasisitiza waislamu kwamba, sherehe ya sikukuu isiwe sababu ya kuwaweka mbali na rehema za Mungu, hivyo kila mmoja achunge nidhamu, ajiheshimu, ajichunge, ajihifadhi na kujisitiri ili kuendelea kupata radhi za Mola.

Pia aliwataka wazazi wawe waangalifu kwa watoto dhidi ya vitendo vya udhalilishaji vinavyoweza kuwatokea katika kipindi cha sikukuu kwa kuwa wahalifu hutumia siku hiyo kuwakatili watoto.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na mgeni wake, Mkurugenzi wa Tamasha la Nchi za Jahazi Zanzibar (ZIFF), Prof. Martin Mhando, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Aonya wanaozorotesha utekelezaji ilani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Hemed Suleiman Abdulla, amesema chama hakitasita kumchukulia hatua mtendaji yoyote wa serikali atakaezorotesha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

Hemed alisema hayo jana wakati akizungumza na viongozi na watendaji wa CCM wa Mkoa wa Kaskazini Pemba katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Alisema katiba na sheria za nchi zinaelekeza kuwa chama kilichoshinda ndicho chenye dhamana ya utekelezaji wa ilani kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Kutokana na maelekezo hayo, alisema, kwa kuwa CCM ndiyo iliyoshinda kupitia uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, viongozi wote walioteuliwa wana jukumu la kuitekeleza ilani hiyo kwa vitendo bila ya kujali itikadi ya chama mtu anachotoka.

Alisema uwapo wa mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, hautoi fursa kwa viongozi wanaotoka vyama vyingine kutotekeleza ilani badala yake inaelekeza kutekeleza ilani ya chama kilichoshinda kwa maslahi mapana ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar katika kuwaletea maendeleo. Mjumbe huyo ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, alisema bajeti iliopitishwa hivi karibuni na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ina lenga kutekeleza ilani ya CCM na kuwataka viongozi wa chama kutoa ushirikiano wa karibu katika kuhakikisha pesa zilizopangwa kutekeleza bajeti hiyo zinatumika ipasavyo.

Hemed aliwashauri viongozi wa majimbo na watendaji wa chama kuchukua jitihada za makusudi kwa kushuka ngazi za chini kwenda kuzungumza na mabalozi kwa lengo la kujenga uhai wa chama.

Pia alisema kitendo cha kusubiri kukaribia kwa uchaguzi hatimaye kuanza kujitokeza kwa kuwafikia wananchi, hakina tija badala yake wanapaswa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao kujishusha ili kutatua matatizo na kero zinazowakabili wananchi.

Hemed aliwataka viongozi hao wa kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba kufanya kazi kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia kwa kuhakikisha wanaweka takwimu sahihi juu ya wanachama kuanzia ngazi ya mashina, matawi, majimbo, wilaya hadi mkoa.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mberwa Hamad Mberwa, alimhakikishia Hemed kuwa uongozi wa chama mkoa utayafanyia kazi maagizo yote alioyatoa kwa lengo kukiimarisha chama.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTELEWA NA CHETI



**INNOCENT P KIBONA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.2655/0137** KILICHOTOLEWA MWAKA 2018 NA BARAZA LA MITIHANI TANZANIA KUPITIA SHULE YA SEKONDARI MARANATHA.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/354428/2021**

116366302

## CAVEAT EMPTOR
**PLOT Nos. 30 & 31, BLOCK 'L' UHURU STREET, MWANZA TOWNSHIP**

**TAKE NOTICE FINNALY** that any person (s) interfering with the said parcels of land as aforesaid stand to lose his/their money as Kelfen Makune Seleman or/and Agnes Festo Makune will neither honor agreements, contact or arrangements entered with person (s) purporting to have authority to transact the parcels of land whether in the manner above described or in any other manner whatsoever nor will it reimburse any monies paid to respect of such transactions.

Dated at Mwanza this 12th day of July, 2021.

Kelfen Makune Seleman

Agnes Festo Makune

116366502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**EMMANUEL IKOLONGO SANGALALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari iliyokuwa na namba ya usajili **T 366 DDH** yenye chasis namba **NCP600227246** injini namba **2NZ3736735.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/360303/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA SINGIDA**
**KITUO CHA UTEMINI**
**MKOA WA SINGIDA**

**SHAURI LA NDOA NAMBA 36 LA 2021**

**ENIGHENJA SYLVANUS MSHANA..........MDAI**

**DHIDI YA**

**WILLBRIGHT VAILECK MLINGI.............MDAIWA**

**MADAI YA TALAKA**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMEFUNGUA SHAURI DHIDI YAKO KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA SINGIDA KITUO CHA UTEMINI KWA MADAI YA TALAKA.
UNAAMRIWA NA MAHAKAMA HII: UHUDHURIE MBELE YA MAHAKAMA HII TAREHE 02/08/2021 SAA 02:30 ASUBUHI BILA KUKOSA KATIKA SHAURI LILILOTAJWA HAPO JUU NA NILAZIMA KULETA MASHAHIDI WAKO NA HATI ZOTE ZINAZOHUSU SHAURI HILO KWA AJILI YA KUJITETEA KATIKA SHAURI HILO.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA, NA MAAMUZI KUTOLEWA.
IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA MAHAKAMA LEO TAREHE 16/07/2021

**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**UTEMINI - SINGIDA**

116366702 116366802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI Kituo cha SINZA Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na. 193.2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU AGNESS K. BATAO WA SINZA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA LILIAN L. BATAO NA MUGISHA L. BATAO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi 08 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
Marehemu hakuacha wosia.
Imetolewa leo tarehe 20 Mwezi 7 Mwaka 2021.

HAKIMU

116366902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SWAUMU SANYAEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA MARK II** yenye namba za usajili **T 182 AAC,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KAH/RB/369/2021**

116368002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 51/2019**
**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA JINAI NO. 280/2017**
**MKURUGENZI WA MASHITAKA...........MRUFANI**
**DHIDI YA**
**AFANA SHAIBU MBILAMBI............MRUFANIWA**
**KUITWA SHAURINI**
**KWA: AFANA SHAIBU MBILAMBI – LIKOMBE MTWARA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe **26/07/2021 saa 2:30** asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo **tarehe 14/7/2021.**

116367602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 47/2019**
**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA LINDI CASE NO. 220/2018**
**THE DPP.......................................APPELLANT**
**VERSUS**
**JUMA ALLY HAMISI@ MKULUPALILE............ RESPONDENT**
**KWA: JUMA ALLY HAMISI@ MKULUPALILE – MAKONGORO LINDI**

**KUITWA SHAURINI**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 28/07/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24/6/2021.

116367802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 37/2019**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 119/2018, Mahakama ya Wilaya Lindi)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA.......................................MRUFANI**
**Dhidi ya**
**MOSES JAPHET@ MGENI...............MJIBU RUFAA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: MOSES JAPHET @ MGENI – NZOVWE MBEYA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 28/07/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 03/06/2021.

116367702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 33/2019**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 5/2019, Mahakama ya Wilaya Lindi)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA.......................................MRUFANI**
**Dhidi ya**
**SALUM ABDALLAH @ NALIOGO NA WENZAKE................WARUFANIWA**
**KUITWA SHAURINI**
**KWA: SALUMU ABDALLAH @ NALIOGO – MADIGO LINDI**
**ADAMU SAID @ OHIMBA – MADIGO - NYANGAMALA LINDI**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama Kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo **tarehe 26/07/2021 saa 2:30** asubuhi bila kukosa.
Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.
Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo **tarehe 14/07/2021.**

116367902

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rais Goïta anusurika kuuawa msikitini

**Bamako,** MALI

KANALI Assimi Goïta ambaye ni rais aliyeko madarakani tangu Mei 24, mwaka huu, ameponea chupuchupu kuuawa kwa kisu.

Watu wawili wamejaribu kaufanya hivyo jana Jumanne asubuhi, kutaka kumchoma rais huyo wa mpito wa Mali bila mafanikio. Tukio hilo lilitokea wakati wa ibada ya Waislam ya Eid al-Adha, sikukuu ya kuchinja wanyama walio halali, katika Msikiti Mkuu wa Bamako, amebainisha mwandishi wa habari wa shirika la habari la AFP.

Walipoulizwa na shirika la habari la AFP juu kitendo hicho kama jaribio la mauaji ya rais, wasaidizi wake walijibu: "Ndio, kabisa ni kweli."

"Tunachunguza. Mtu mmoja amejaribu kumshambulia kwa kisu katika Msikiti Mkuu wa Bamako leo (jana)," chanzo hicho kiliongeza, kikisema rais yuko salama na mzima.

Akiwa katika eneo la tukio, Waziri wa Masuala ya Kidini, Mamadou Koné, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba, mtu amejaribu katika Msikiti Mkuu wa Bamako kumuua rais wa mpito kwa kisu. Lakini amedhibitiwa kabla ya kutekeleza uhalifu.

"Ilikuwa baada ya sala na mahubiri ya imamu, wakati imamu akijiandaa kwenda kuchinja kondoo wake, ndipo kijana huyo alijaribu kumchoma Assimi Goïta mgongoni, lakini mtu mwingine ndiye alijeruhiwa," Latus Tourè, Msimamizi wa Msikiti Mkuu, amelithibitishia shirika la habari la AFP.

Mali imeshuhudia majaribio mawili ya mapinduzi katika kipindi cha mwaka mmoja, jaribio la kwanza lilifanyika Agosti, mwaka jana na kisha Mei, mwaka huu.

**RFI**



Maofisa polisi wakiangalia gari lililoharibiwa na roketi mjini Kabul, nchini Afghanistan. Roketi kadhaa zilirushwa jana, kulenga Kasri ya rais Kabul ingawa hazikufanikiwa kulenga eneo hilo kwa mujibu wa vyombo vya habari nchini humo. **PICHA: XINHUA**

# Kesi ya Zuma yasogezwa hadi Agosti

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

MAHAKAMA ya Afrika Kusini imekubali ombi la Zuma la kucheleweshwa kwa kesi yake ya ufisadi inayohusu makubaliano ya ununuzi wa silaha, iahirishwe kwa wiki tatu.

Zuma anatuhumiwa kupokea rushwa kutokana na makubaliano ya mauzo ya silaha ya zaidi ya dola bilioni mbili katika miaka ya 1990.

Alikana mashitaka hayo Mei, mwaka huu akiwa ni pamoja na ufisadi, ubadhirifu na biashara haramu ya mzunguko wa fedha.

Alikwepa mashtaka hayo kwa zaidi ya muongo mmoja na akajionyesha kama mwathirika wa ushawishi wa kisiasa.

Jitihada za kumwajibisha zinaonekana kama mtihani wa uwezo wa nchi kuwawajibisha wanasiasa wenye nguvu.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi kuandia tarehe 10 hadi 13 Agosti, mwaka huu, Jaji wa Mahakama Kuu ya Pietermaritzburg Piet Koen alisema. Hakutoa sababu kwanini aliruhusu kusogezwa mbele.

Zuma yuko katika kifungo cha miezi 15 kwa kudharau mahakama.

**VOA**

# Mwanamfalme Saudia awapa vijana 200 mamilioni ya kuoa

**Riyadh,** SAUDI ARABIA

MWANAMFALME wa Saudia, Muhammad Bin Salman ameidhinisha kutolewa kwa pesa milioni 3.74 za riyali, sawa na dola milioni moja za kimarekani, ili zigawiwe kwa vijana 200 kama ruzuku ya kuoa.

Gazeti la serikali la Saudi Arabia limeripoti kwamba tangazo hilo lilitolewa na Shirika la habari la Saudia, mwishoni mwa wiki.

Taarifa hiyo ilisema kuwa fedha hizo zitagawanywa kwa vijana wa kiume na wa kike kote nchini humo.

Lilisema agizo la mwanamfalme huyo ni katika juhudi za kuwasaidia yatima na watu wenye ulemavu, ambao wamekuwa na shida ya kuoa.

Katika awamu ya kwanza ya mpango huo, riyali milioni 250 za msaada zilisambazwa, kwa watu zaidi ya 26,000 kutoka maeneo tofauti ya nchi hiyo.

Licha ya kupewa pesa, vijana watafundishwa jinsi ya kutumia pesa.

Mpango wa Mwanamfalme Muhammed Bin Salman ulianzishwa kwa lengo la kuimarisha uchumi na jamii ya watu wa nchi hiyo kuboresha maisha ya watu.

**BBC**

## Uholanzi kuipatia Tanzania chanjo corona Astrazeneca

**Amsterdam,** UHOLANZI

UHOLANZI itatoa chanjo ya corona kwa nchi chache za Afrika, ikiwamo Tanzania kupitia mpango wa chanjo unaosimamiwa na Serikali.

Uholanzi imetenga dozi 750,000 za chanjo aina ya Astrazeneca kwa ajili ya nchi zenye mahitaji ikiwamo Tanzania na Namibia.

Dozi hizo zimehifadhiwa tayari kwa ajili ya kusambazwa kwa nchi hizo zilizoonyesha nia ya kusaidiwa.

Uholanzi kupitia mamlaka zake za afya inachangia chanjo kusaidia nchi masikini kukabiliana na virusi vya corona, ikifanya hivyo pia kwa kuchangia karibu dozi nusu milioni kwenye mpango wa chanjo kwa nchi masikini (COVAX).

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu, Uholanzi inatarajiwa kuchangia dozi milioni 20 kwenye mpango huo.

Kwa mujibu wa tovuti ya Uholanzi mbali na Tanzania, Cape Verde na Indonesia ni miongoni mwa nchi zilizonufaika na hatua hiyo.

Mapema mwezi huu, Uholanzi ilitangaza kuipa Indonesia dozi milioni tatu za chanjo hiyo, ingawa haijafahamika wazi, ni kiwango gani cha chanjo zitapelekwa Tanzania na Namibia.

Serikali ya Uholanzi imeeleza kuwa, wizara yake ya afya itasimamia usambazaji kuzifikia nchi hizo.

**BBC**

## Wavamizi bunge la Marekani wahukumiwa

**Washington,** MAREKANI

KWA mara ya kwanza hukumu ya kifungo cha gerezani imetolewa kwa mtu aliyehusika na uvamizi wa jengo la bunge na umwagaji damu mnamo Januari 6 katika nchi ya Marekani.

Paul Hodgkins mwenye umri wa miaka 38, alisema kwa alijutia hatua hiyo kortini, ambapo alishtakiwa kwa kuvamia jengo la bunge na kuzuia utendaji kazi wa wabunge.

Mwendesha Mashtaka wa serikali Randolph Moss alibaini kuwa Hodgkins alifanya shambulizi kubwa kwa demokrasia, ingawa alikiri kosa, alipunguziwa hukumu ya kifungo cha miezi 18 gerezani kilichopendekezwa na waendesha mashtaka.

Hodgkins alihukumiwa kifungo cha miezi nane gerezani na mahakama.

Ilielezwa kuwa hukumu iliyotolewa kwa Hodgkins Florida inaweza kuwa kielelezo kwa takriban wafuasi 230 wa rais wa zamani wa Marekani Donald Trump ambao walizuiliwa kwa sababu ya uvamizi wa bunge Januari 6, mwaka huu na wanasubiri kuhukumiwa kwa shtaka moja.

**TRT**



# DEPAY afurahia kusajiliwa Barca

**BARCELONA, Hispania**

MEMPHIS Depay amewasili rasmi Barcelona kabla ya mazoezi yake ya kwanza jana Jumanne asubuhi, mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi amethibitisha kuwa anafurahi sana kwa safari mpya.

Memphis amesaini na klabu hiyo ya Katalunya kwa makubaliano baada ya mkataba wake na Lyon kumalizika, na kocha Ronald Koeman alitoa kwa Blaugrana hao kupata saini yake.

Baada ya kutua huko Barcelona, mchezaji huyo wa zamani wa Manchester United amejitambulisha kwa mashabiki na kuonyesha furaha yake.

"Jamani mimi ni Memphis, nimefika hapa Barcelona na ninafurahi sana kupata changamoto mpya, safari mpya na natumai kuwaona nyinyi hivi karibuni uwanjani," aliandika Memphis kwenye ukurasa wake wa Instagram.

Mchezaji huyo pia alizungumzia jinsi anavyotarajia kushinda mataji mengi klabuni hapo, huku akimshukuru Koeman kwa msaada wake.

"Koeman alinipa ujasiri wakati nilipoumia mpaka kupona kwangu," aliandika Memphis juu ya kocha wake huyo wa zamani wa timu ya taifa ya Uholanzi.



# ARSENAL, DEST WAFANYA MAZUNGUMZO

**LONDON, England**

ARSENAL wameripotiwa kuwa wamefanya mawasiliano na beki wa kulia wa Barcelona, Sergino Dest, wakati kukiwa na uvumi juu ya hatima ya Hector Bellerin.

Bellerin ameonekana kama beki wa kulia wa chaguo la kwanza pale Arsenal chini ya Arsene Wenger, Unai Emery na Mikel Arteta, lakini alipoteza jukumu hilo kwa Calum Chambers mwishoni mwa msimu uliopita.

Hivyo, Bellerin anaripotiwa kushinikiza kuhamia Inter Milan, na Arteta atatafuta mbadala wa nafasi ya raia huyo wa Hispania wakati wa msimu mgumu wa kifedha hapo Arsenal.

Washika bunduki wametajwa kutaka kumsajili Max Aarons wa Norwich City kama mbadala wa Bellerin, lakini pia kwa mujibu wa Sky Sport, washikabundi hao wamegusa dili la msingi la nyota wa Barcelona kuangalia uwezekano wa uhamisho wa dau la pauni milioni 25.7 kwa Dest.

Ripoti hiyo imeongeza Bayern Munich na Juventus pia walitajwa kuwa na nia kwa mchezaji huyo wa zamani wa Ajax, lakini hana mpango wa kuondoka Barcelona baada ya kujihakikishia nafasi yake chini ya kocha Ronald Koeman.

Dest alifunga mabao matatu na usaidizi wa bao moja kwenye mechi 41 za mashindano yote ya msimu uliopita, na mkataba wake pale Camp Nou unadumu hadi 2025.

# Bayern yawanyatia mabeki Barcelona

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich wanahitaji kujiimarisha katika nafasi ya beki wa kulia na wanavutiwa na uwezekano unaotolewa na Barcelona, ambao wana mabeki wakubwa watatu wa kulia ambao wanahitaji sana kuleta fedha klabuni hapo.

Klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundelsiga imeripotiwa kuwaulizia mabeki Sergino Dest, Emerson na Sergi Roberto.

Hiyo ni kwa mujibu wa RAC1, ambao wanaelezea kuwa Dest litakuwa chaguo linalopendelewa na Bavaria hao.

Hata hivyo, Bayern Munich kama itamkosa Dest ipo tayari kutoa ofa kwa Emerson au Sergi.

Kocha Ronald Koeman pia hana tatizo kuwabakisha wote, wakati pia wachezaji wenyewe inasemekana wanapenda kubakia hapo Camp Nou.

Wakati wa kuangalia uwezekano wa kuondoka katika nafasi ya ulinzi ni Samuel Umtiti na Clement Lenglet ambao ndio wachezaji wanaotarajiwa kuondoka.



## HABARI MICHEZO

# Atletico yatangaza kutomuuza Joao Felix

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Atletico Madrid haitarajii kufanya uamuzi wa kumuuza kiungo wake, Joao Felix kwenye dirisha hili la uhamisho.


Jina la Felix limekuwa likitajwa sana kwenye taarifa mbalimbali za masuala ya uhamisho wa wachezaji, baada ya kuwa na msimu wenye panda shuka tangu alipowasili klabuni hapo kwa pauni milioni 127 mwaka 2019.

Kutokana na ada kubwa aliyolipiwa nyota huyo amekuwa akikosolewa kwa urahisi zaidi na watu wengi licha ya ukweli kuwa bado anaendelea kujiboresha kama mchezaji.

Felix amefanikiwa kupata mabao 10 na asisti sita wakati Atletico wakifanikiwa kushinda taji la LaLiga msimu uliopita.

Atletico wanatarajia nyota huyo ataendelea kujiboresha kuwa bora zaidi, na kwa mujibu wa Marca, Felix atakuwa hashikiki kwenye dirisha hili la uhamisho huku klabu ikiwa imepania kumtumia vyema msimu unaokuja.

Hivyo, mpango wa klabu ni kumpa muda wa kuendelea kujiboresha na mpango wa kumweka sokoni haupo kabisa mezani kwa sasa.



# ARSENAL yakamilisha usajili wa Lokonga

**LONDON, England**

ARSENAL imekamilisha usajili wa kiungo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji chini ya umri wa miaka 21, Albert Sambi Lokonga kutoka klabu ya Anderlecht.

Miamba hao wa Ligi Kuu England walitangaza kumsajili Lokonga na kwamba amesaini mkataba wa "muda mrefu", na ingawa ada yake haijawekwa wazi, lakini imeripotiwa ni pauni milioni 15 ambayo ni ya awali.

Lokonga mwenye umri wa miaka 21, ni zao la akademi ya vijana ya Anderlecht ambayo iliwaibua wachezaji kama Romelu Lukaku, Youri Tielemens na Leander Dendoncker na alicheza mechi 78 kwa klabu yake.

"Ni uhamisho mkubwa kwa sababu nimekuwa nikicheza pale Anderlecht kwa miaka 10," alisema Lokonga akinukuliwa na tovuti rasmi ya Arsenal.

"Ni hatua kubwa, lakini najihisi kujiamini kwa sababu soka la dunia tayari limeniamini.

"Nasubiri kwa hamu kuanza kucheza kwenye Ligi Kuu England na kuanza kuonekana, kwa hakika ni jambo zuri kwangu.

"Mwanasheria wangu aliniambia kuhusu nia ya Arsenal na sikusita hata mara moja. Nilisema, 'samahani, nitakwenda pale'."

Arsenal tayari amemsajili kinda mwingine mwenye umri wa miaka 21, Nuno Tavares kutoka Benfica ambaye anacheza nafasi ya mlinzi wa pembeni.




# WAKALA WA GRIEZMANN AMPELEKA EPL

**BARCELONA, Hispania**

WAKALA wa mshambuliaji wa Barcelona, Antoine Griezmann ameripotiwa kufanya mazungumzo na timu zinazoshiriki Ligi Kuu England, wakati kukiwa na uvumi kuhusu sintofahamu ya hatua anayoenda kuichukua ya Mfaransa huyo.

Pamoja na Barcelona kuwa chini ya shinikizo kubwa la kupunguza mzigo wa matumizi ya fedha kwenye dirisha la sasa, Griezmann anaeleweka kuwa moja ya majina kadhaa yaliyowekwa kwenye mpango wa kupunguzwa.

Atletico Madrid wamehusishwa sana na mshambuliaji wao huyo wa zamani kama sehemu ya makubaliano ya kubadilishana yanayomuhusu Saul Niguez, lakini hakuna ushahidi kuwa kuna makubaliano yoyote juu ya pendekezo kama hilo.

Chelsea wanahusishwa na nia ya kumchukua Griezmann kwa mkopo, wakati Manchester City, Liverpool, Juventus, Paris Saint-Germain na Bayern Munich zote zikitajwa kuwa windoni dhidi ya saini ya nyota huyo, lakini Atletico bado wanaendelea kuongoza orodha hiyo.

Barcelona wanatajwa kusita kufanya uamuzi juu ya hatma ya Griezmann, ambaye amejitahidi sana akiwa na Barcelona, akiwa na idadi nzuri ya mabao 20 na asisti 13 kwenye michezo 51 ya mashindano yote msimu uliopita.

## KWA UFUPI

### HENDERSON HAKIELEWEKI
MUSTAKABALI wa Jordan Henderson mwenye umri wa miaka 31 katika klabu ya Liverpool haueleweki, mazungumzo ya mkataba mpya na nyota huyo wa England yameshindwa kuendelea tangu kumalizika kwa msimu. ***(The Athletic)***

### RICE ANUKIA CHELSEA
CHELSEA inafahamu kiungo wa England na West Ham United, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, ana nia ya kujiunga nao na watawasiliana na wagonga nyundo hao kujua nini cha kufanya ili kukamilisha mpango huo. ***(Express)***

### CITY YAMTAKA MENDES
MANCHESTER City wanamtaka mlinzi wa kushoto wa Sporting Lisbon na Ureno, Nuno Mendes mwenye umri wa miaka 19, lakini hawako tayari kutoa kitita cha pauni milioni 50 ili kumnasa nyota huyo. ***(Fabrizio Romano)***

### ATLETICO YAMBANA TRIPPIER
ATLETICO Madrid wanaendelea na msimamo wao kwamba, beki wake raia wa England, Kieran Trippier (30), hauzwi licha ya Manchester United kuonyesha nia ya kumtaka, lakini klabu hiyo ya Hispania huenda ikamsajili beki wa kulia wa Wolves na Ureno Nelson Semedo (27), au beki wa kulia wa Napoli na Italia, Giovanni di Lorenzo mwenye umri wa miaka 27, iwapo Trippier ataamua kuondoka. ***(AS)***

### SPURS YAMWANIA ROMERO
TOTTENHAM Hotspur ipo katika mazungumzo mazuri na Atalanta kuhusu uhamisho wa beki wa kati wa Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 23. ***(Football.London)***

### LOCATELLI AGOMBEWA
ARSENAL hadi sasa wako kando katika harakati zao za kumshawishi kiungo wa Italia, Manuel Locatelli, licha ya utayari wao wa kulipa dau la pauni milioni 34 linalotakiwa na Sassuolo, huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 23 akijiandaa kuichagua Juventus kutokana na kushiriki kwake kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mirror)***

### VARANE AIOTA EPL
MLINZI wa kati wa Real Madrid na Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28, yuko tayari kutua katika Ligi Kuu England huku Manchester United wakiwa na nafsi kubwa ya kumsajili. ***(Guardian)***


### DE BEEK KUTUA BARCA
BARCELOAN wamepewa fursa ya kumsajili kiungo wa Manchester United na Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24, wakati klabu hiyo ya Hispania pia ikimtumia beki wake, Samuel Umtiti mwenye miaka 27, kama sehemu ya mpango huo. ***(Sport via Express)***

### UNITED YAVAA KIGINGI
MMILIKI wa Napoli, Aurelio de Laurentiis, amekataa dau la pauni milioni 30 lililotolewa na Manchester United kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa klabu hiyo, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 30. ***(Gazzetta)***

### CAMAVINGA NJIA MOJA
MANCHESTER United wako tayari kuvuta subira katika harakati zao za kumshawishi kiungo wa Rennes, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, wakati huu wanapojaribu kupunguza dau lake. ***(The Athletic)***

### POGBA, MBAPPE HURU
KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, mshambuliaji wa Juventus na Ureno Cristiano Ronaldo (36), na straika wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe (22), ni miongoni mwa wachezaji wanaoweza kuwa huru msimu ujao, kutokana na athari za janga la corona zilizozikumba klabu zao. ***(ESPN)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID YAJIANDAA KUMUUZA HAZARD

**Hata hivyo kocha wake Ancelotti ameonyesha nia ya kuhitaji kufanya...**

**MADRID, HISPANIA**

KIUNGO mshambuliaji wa Real Madrid, Eden Hazard, ameripotiwa kuwekwa sokoni na miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Nyota huyo wa zamani wa Chelsea amevumilia wakati mgumu wa kuuguza majeraha ya mara kwa mara tangu alipowasili katika mji mkuu wa Hispania, Madrid akitokea England, akicheza mechi 43 tu akiwa na Real kwa misimu miwili iliyopita.

Hazard amekuwa akihusishwa na kurejea Chelsea wakati akiendelea kupambania nafasi yake ndani ya Real Madrid, lakini amethibitishwa anataka kuwa kinara huko Bernabeu.

Hazard amekuwa akipambana na majeraha tangu alipowasili Real Madrid kutoka Chelsea.

Hata hivyo, gazeti la Marca inaripoti Real Madrid imejiandaa kumweka Hazard sokoni kwenye dirisha hilo la uhamisho wa majira ya joto licha ya nia ya kocha mpya, Carlo Ancelotti kutaka kufanya kazi na raia huyo wa Ubelgiji.

Ripoti hiyo inadai kwamba Ancelotti ana uhakika kuwa anaweza kumtumia vyema mshambuliaji huyo aliyetawaliwa na majeraha misimu miwili mfululizo iliyopita, lakini Real Madrid wanaweza kumuuza ikiwa watapata mnunuzi kwa bei sahihi.

Hazard ameona nyavu mara tano tu tangu alipowasili Real Madrid, na alitoa msaada wa bao moja katika mechi nne za Ubelgiji kwenye Euro 2020 iliyomalizika wiki iliyopita.

Hadi sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, hakuna klabu ambayo imeonyesha nia ya wazi ya kutaka kumsajili Hazard katika kipindi hiki cha usajili.

Ingawa mwenyewe ameshaonyesha ishara wazi kuwa kama akiondoka hapo Real Madrid kituo chake kinachofuata ni klabu yake ya zamani ya Chelsea.

## HABARI MICHEZO

# COASTAL UNION, PAMBA VITANI KUCHEZA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

MECHI mbili za mchujo kutafuta timu zitakazocheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2021/22 zinatarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza kwa Pamba kuikaribisha Coastal Union huku kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Transit Camp itawavaa Mtibwa Sugar.

Coastal Union na Mtibwa Sugar zinacheza mechi za mchujo maarufu kama 'play off', baada ya kushika nafasi ya 13 na 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika Jumapili iliyopita, zikiepuka kushuka daraja moja kwa moja, lakini hatima zao zikiwa kwenye mechi hizo.

Iwapo zitafanya vizuri kwenye mechi hizo na zile za marudiano Jumamosi, zitabaki kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini kama zitafanya vibaya, zitashuka daraja na kucheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara msimu ujao.

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno, alisema wanashukuru kupata nafasi ya kucheza mechi za mchujo baada ya kikosi chao kuwa na msimu 'mgumu' kutokana na matokeo mabaya waliyokuwa wanapata.

Mgweno alisema Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ilikuwa na ushindani zaidi lakini wanashukuru matokeo chanya ya mechi mbili za mwisho ndio yaliyowasaidia kucheza hatua hiyo ya mchujo.

"Sisi ndiyo tulikuwa kwenye hali mbaya zaidi kwa sababu tulikuwa wa pili kutoka mwisho kwenye raundi mbili za mwisho. Yaani kutoka Mwadui ambayo imeshuka moja kwa moja, tukawa sisi. Kwa vyovyote vile tumejitahidi sana hadi kutoshuka daraja na kucheza 'play off.'

Alisema kuwa wamejipanga kuhakikisha wanabaki Ligi Kuu, hivyo wana uhakika kuwa kushinda mechi ya leo japo alisema itakuwa ngumu.

"Kwa kujipanga na mechi hii, ndiyo maana unaona tumekuja (Mwanza), kwa ndege ili kutowachosha wachezaji wetu," alisema kiongozi huyo.

Pamba, Mabingwa wa Ligi Kuu ya Muungano mwaka 1990, itakuwa ikijaribu kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushuka daraja katikati ya miaka ya 1980.

Timu hiyo imekuwa kwenye majaribio kadhaa ya kutaka kurejea, lakini imekutana na wakati mgumu mara kadhaa, kwani msimu wa 2018/19, ilikaribia kufanya hivyo, lakini ikafungwa mabao 2-0 na Kagera Sugar kwenye mechi ya 'play off' ugenini, baada ya kutoka suluhu nyumbani.

Transit Camp, itakuwa inajaribu kuondoa 'gundu', kwani ni timu inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza kwa muda mrefu baada ya kushindwa 'kuzichanga' vyema karata zake.

Tayari Geita Gold FC ya Shinyanga na Mbeya Kwanza zimeshapanda daraja baada ya kuibuka vinara katika makundi yao.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 23 (U-23), wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa JMK Park jijini Dar es Salaam jana asubuhi kwa ajili ya kuelekea Ethiopia katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA). Kikosi hicho kitashuka dimbani leo kucheza dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). **PICHA: TFF**

# Wanariadha Dar kuchuana Agosti

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Riadha Mkoa wa Dar es Salaam (DAAA), kimetangaza rasmi mashindano yake yatafanyika Agosti 13 na 14, mwaka huu jijini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Msaidizi wa DAAA, Felix Chunga, alisema maandalizi ya mashindano hayo yanaendelea vyema na jumla ya wanariadha 20 wanatarajia kuchuana.

Chunga alisema wiki ijayo wanatarajia kufanya mchujo ili kupata wanariadha hao ambao watachuana katika ngazi ya mkoa.

"Maandalizi ya mashindano yetu yanaendelea vizuri na tunatarajia kufanya mchujo wa wanariadha ifikapo mwishoni wa mwezi huu, nina imani kila kitu kitakwenda vizuri na malengo yetu yatatimia,"alisema Chunga.

Katibu huyo alisema mashindano hayo yana lengo la kuendelea kuinua vipaji vya wanariadha wa hapa jijini lakini pia DAAA ikiwaomba wadau wa mchezo huo wajitokeze kuunga mkono mashindano hayo ambayo yanatarajiwa kuwa na ushindani.

"Tunawakumbusha wanariadha wote watakaopata nafasi ya kushiriki mashindano haya kujituma na hatimaye kupandisha viwango vyao jambo ambalo litawasaidia kukaa kwenye orodha nzuri ya mkoa kuelekea michuano ya kitaifa itakayofanyika hapo baadaye," Chunga alisema.

Hata hivyo Chunga alisema hamasa zaidi inahitajika katika mchezo huo ambao kwa sasa umaarufu wake umeshuka tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

## Kiduku ajipanga kumpiga Mbabe

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa kutoka mkoani Morogoro, Twaha Kiduku, amesema anaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na pambano dhidi ya Abdallah Pazi (Dula Mbabe) litakalofanyika Agosti 20, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kiduku alisema kwa sasa anafanya mazoezi ya kutengeneza mji na kambi yake iko nje ya mji.

"Ninaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na mpinzani wangu, ninaomba mashabiki wa Mkoa wa Morogoro waniombee ili nifanye vizuri katika pambano hilo, nimeamua kujificha nje ya mji kwa ajili ya kukimbia kelele za watu,"alisema Kiduku.

Bondia huyo alisema licha ya pambano hilo kuwa na ushindani, anaamini atapata ushindi kwa sababu amejipanga vizuri na anamfahamu vyema mpinzani wake huyo.

"Naomba mashabiki wangu msiwe na hofu, ninaahidi nitafanya vizuri katika pambano hili, ninawaomba wajitokeze kwa wingi siku ya mchezo ili waweze kushuhudia burudani nitakayoitoa siku hiyo," alisema bondia huyo.

Naye Kocha wa Kiduku, Pawa Iranda, alisema hana wasiwasi na bondia wake kutokana na kiwango kizuri alichokuwa nacho kilichoimarishwa na mazoezi magumu anayofanya.

## Njombe watakiwa kuandaa michuano

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

WADAU wa soka wa Mkoa wa Njombe wametakiwa kuanzisha mashindano mbalimbali ya mchezo huo kwa ajili ya kuibua na kuendeleza vipaji vya wachezaji vijana, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Gwakisa Kasongwa amewaomba wadau wa michezo wilayani hapa kuhakikisha wanaandaa michuano ili kusaidia kunyanyua sekta ya michezo mkoani Njombe.

Kasongwa alisema hayo katika uzinduzi wa mashindano ya Kombe la Luwanja uliofanyika katika Kata ya Mtwango ambapo umetoa nafasi ya vijana kuonyesha vipaji pamoja na kudumisha afya zao.

Kiongozi huyo alisema michuano kama hiyo husaidia kupata wachezaji wazuri ambao baadaye husaidia klabu na taifa kufanya vyema kwenye mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

"Nitoe pongezi hizi kwanza kwa mwazilishi wa ligi, nitoe wito kwa vijana kuitikia ligi hizi na kuona kama ni fursa kwa sababu kuanzia kwenye ligi hizi ndio tunawapata kina Mbwana Samatta, kwa hiyo lazima tuanzie huku chini, hii ni ajira," alisema kiongozi huyo.

Michezo
Jumatano Julai 21, 2021
Nipashe




MADRID YAJIANDAA KUMUUZA HAZARD HABARI UK 22




Mbunge wa Dodoma Mjini (CCM), Anthony Mavunde (wa pili kushoto), akikabidhi tuzo ya shukrani kwa wachezaji wa Yanga kwa kumaliza salama msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21 katika sherehe maalumu iliyoandaliwa na Umoja wa Matawi ya Yanga jijini Dodoma iliyofanyika Jumapili iliyopita. PICHA: MTANDAO

# YANGA YASISITIZA HAITABEBWA CAF

## ●●● Inatamba imejiimarisha kutwaa Kombe la FA na...

**Na Saada Akida**

HUKU zikiwa zimesaliwa siku nne kuelekea fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma, mabosi wa Yanga wamesema watapambana kuhakikisha wanashiriki michuano ya kimataifa kwa uwezo wao na si kupitia watani zao Simba.

Kikosi cha timu hiyo kinatarajiwa kuondoka jijini Dar es Salaam kesho kuelekea mkoani Kigoma tayari kwa ajili ya fainali hiyo itakayotoa mwakilishi wa mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa alisema timu yake imejipanga vizuri kuelekea fainali hiyo ambayo inasubiriwa kufunga rasmi msimu wa 2020/21 hapa nchini.

Mfikirwa alisema ana imani na kikosi hicho na wameamua kwenda Kigoma mapema ili wachezaji wao wapate nafasi ya kuzoea mazingira ya mji huo pamoja na kufanya mazoezi kwenye uwanja wa Lake Tanganyika ambao ni mgeni kwa nyota wake.

"Tunaendelea na maandalizi katika kiwango cha juu ikiwamo kuwahi kufika Kigoma mapema ili kuandaa mazingira bora ya timu, sehemu ya kufanyia mazoezi na kufikia wachezaji wetu, kwa upande wa uongozi tuna imani na vijana wetu, kikosi kipo fiti kwenda kutafuta ushindi katika fainali hiyo," alisema Mfikirwa.

Kiongozi huyo alisema wamejipanga kwenda kuendeleza rikodi ya kuwafunga wapinzani wao kwa mara ya pili katika ardhi ya Bongo.

"Siku zote tunasema kuwa fainali haichezwi bali fainali hushindwa, hivyo kuelekea katika mchezo huo, tunaenda kwa ajili ya kushinda fainali hiyo na kila kitu kinaenda vizuri na tutapata ushindi," alisema Kaimu Katibu huyo.

Aliongeza hawakubali kwenda kucheza michuano ya kimataifa kupitia 'mgongo' wa Simba, wanahitaji kupambana kushinda katika fainali na kutwaa taji la ubingwa wa Kombe la FA.

Kuhusu tetesi za usajili kwa wachezaji wapya huku wakihusishwa mshambuliaji kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Fiston Mayele na Heritier Makambo, alikataa kusema lolote na kuongeza masuala ya usajili bado yako chini ya kamati husika ambayo inafanya kazi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Kocha wao Nesreddine Nabi.

"Jana (juzi), Kamati ya usajili ilikutana kujadili majina ya wachezaji waliopendekezwa, kwa sasa tuko makini katika suala la usajili, hatuwezi kurudia makosa ya msimu uliopita," Mfikirwa alisema.

Naye Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli aliliambia gazeti hili timu yao bado haijapata straika kwenye uwezo mkubwa wa kupachika mabao kama walivyokuwa na Mkongomani Heritier Makambo.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema wanachama na mashabiki wa timu hiyo wanamkumbuka Makambo kutokana na uwezo wake kupachika mabao alipokuwa katika kikosi chao kwenye msimu wa 2018/19, kabla ya kwenda kujiunga na Horoya ya Guinea.

# MANULA AIOTA TUZO YA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA chaguo la kwanza la mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Aishi Manula amesema ameshafanya kila kitu kwenye soka la hapa nchini na sasa akili yake anaielekeza kuwania tuzo ya mlinda mlango bora wa Afrika.

Manula ambaye alitua Simba akitokea Azam FC mwaka 2017, pia ndiye golikipa namba moja wa Timu ya Soka ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars).

Nyota huyo alisema hayo wakati akizungumzia mafanikio yake baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 iliyomalizika Jumapili iliyopita, ambapo huu ni msimu wa sita mfululizo anashinda tuzo hiyo baada ya kuongoza kwa kutoruhusu mabao kwenye mechi nyingi kuliko makipa wengine.

"Huu ni msimu wa sita mfululizo sasa naongoza kwa 'clean sheet', na kuwa kipa bora. Nimeshazoea sasa na hata shabiki yoyote au wanahabari wakisikia Manula kipa bora hakuna anayeshtuka kwa sasa. Kila mtu anaona kawaida. Hata mimi mwenyewe naona kawaida, " alisema Manula.

**Alisema lengo lake kwa sasa ni kushindana na magolikipa wakubwa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na kutwaa tuzo ya kipa bora wa Afrika.**

"Sasa nataka niende juu kidogo kwa sababu huku chini nimeshamaliza, ninataka nishindane nipate 'clean sheet' za kutosha kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ili nichukue tuzo huko," alisema golikipa huyo.

Manula amemaliza Ligi Kuu Tanzania Bara 2020/21 akiwa na 'clean sheet' 18, akifuatiwa na kipa wa Mbeya City, Haroun Mandanda ambaye amesimama golini mara 15 bila kuruhusu wavu wake kutikiswa huku Metacha Mnata wa Yanga na Abutwalib Mshery wa Mtibwa Sugar, wana 'clean sheet' 13 kila mmoja.

Kipa mkongwe, Juma Kaseja, yeye amesimama langoni mara 11 bila kuruhusu bao pamoja na Aaron Kalambo wa Dodoma Jiji, huku Daniel Mgore wa Biashara United akiwa na 'clean sheet' 10.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002